






**NEMC** yaitoza faini bil.3.3/- kampuni ya mafuta kukiuka sheria

UKURASA 19







# Nipashe

Jumanne Septemba 7, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580696

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


### KESI YA MBOWE

# JAJI AJIENGUA

**Ni** baada ya mshtakiwa kumtaka afanya hivyo kwa kumpa hoja tatu...*Endelea ukurasa 2*



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna, wakizindua NMB Foundation jijini Dar es Salaam. Kushoto ni Naibu Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mwanaidi Ali Khamis na kulia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa NMB, Dk. Edwin Mhede. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## IGP, vyama vya siasa, msajili uso kwa uso



UKURASA 5

UKURASA WA 5

### PM: TAASISI ZA SERIKALI TOENI HUDUMA PAMOJA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameziagiza taasisi za serikali ambazo hazijaanza kutoa huduma kupitia vituo vya Huduma Pamoja vya Shirika la Posta Tanzania zihakikishe zinaanza...

UKURASA WA 5

### MADAKTARI WALAANI TUKIO LA MGONJWA KUFUMULIWA NYUZI

CHAMA cha Madaktari Tanzania (MAT) kimelaani vikali kitendo kilichofanywa na daktari wa Kituo cha Afya Kerege wilayani Korogwe...

UKURASA WA 19

### ADAIWA KUUA MUME KWA DAWA AACHE KUNYWA POMBE

JESHI la Polisi mkoani Tabora linamshikilia mwanamke aitwaye Mbaru Mwagembe, kwa tuhuma za kusababisha kifo cha mumewe...

UKURASA WA 19

### WIKI 1 TANI 100,000 MAHINDI ZINUNULIWE

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimetoa wiki moja kwa serikali kununua tani 100,000 za mahindi kutokana na baadhi ya wakulima...

## Bosi PAC: Kuna shida uteuzi wa mawaziri, watendaji

UKURASA 4

**MICHEZO** AZAM WALIA RATIBA FIFA KUWATIBULIA ZAMBIA UK.23

**MAONI, KATUNI** UK.6



Kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Zuberi Kabwe (katikati), akiwa amezuiwa kuingia katika Mahakama ya Mafisadi iliyopo Mawasiliano Sinza jijini Dar es Salaam jana, kusikiliza kesi ya Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Jaji ajiengua kesi ya Mbowe

**Na Kulwa Mzee**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amemwomba Jaji Elinaza Luvanda kujitoa kusikiliza shauri lao, ili kujenga heshima yake, heshima ya Mahakama na asibebeshwe lawama, ambazo pengine hazikustahili.

Jaji Luvanda amesema hawezi kujitetea kwa jambo ambalo halipo, amekubali kujitoa na amesema shauri lina maslahi mapana ya umma anaona ni busara akae pembeni.

Tukio hilo lilitokea jana Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi baada ya kumaliza kutoa uamuzi wa mapingamizi yaliyowekwa na upande wa utetezi wakidai hati ya mashtaka ina kasoro.

Katika uamuzi wake Jaji Luvanda alikubaliana na hoja moja ya pingamizi na kutupilia mbali hoja mbili.

Akisoma uamuzi alisema msingi wa pingamizi ni makosa yaliyofunguliwa chini ya kifungu namba 4(3) cha Sheria ya Ugaidi Namba 21 ya Mwaka 2002, haikueleza malengo wakati ndio msingi wa makosa ya ugaidi kwa shtaka namba 1, 4, 6.

"Maoni yangu kwamba hoja hii inachukua muda mrefu sana, marejeo yalipaswa kufanywa katika hansad za Bunge, kuona michango ya wabunge wakati sheria hiyo inatungwa kuona kama walitoa tafsiri ya ugaidi, bila kuhusisha itikadi za dini na siasa.

"Majibu yanapatikana katika hansad, sipendi kuhitimisha katika hatua za awali, itafutiwe hoja nzito zaidi itatolewa uamuzi huko baadaye," alisema Jaji Luvanda.

Jaji Luvanda alisema Mahakama inakubaliana na hoja moja ya upande wa utetezi kwamba shtaka namba 1, 4, 6 yaliyofunguliwa chini ya kifungu namba 4(3) cha Sheria ya Ugaidi ilikuwa ni sharti kutumia maneno yaliyolengwa chini ya kifungu hicho.

Alisema anakubaliana na hoja ya Wakili Peter Kibatala kwamba, ili kuweka tofauti hayo maneno yanaweka mpaka baina ya makosa ya ugaidi na makosa mengine ya jinai.

Baada ya kusema hayo alitupilia mbali hoja mbili na alikubali hoja moja akatoa maelekezo kwa upande wa Jamhuri kufanyia mabadiliko shtaka namba 1, 4 na sita.

Mshtakiwa Mbowe aliomba kuzungumza na Mahakama ilimruhusu kufanya hivyo.

Mbowe alisema washtakiwa wote wanatumaini uamuzi unaotolewa usipotekelezwa kwa mujibu wa sheria na sheria ikaonekana imetumika wanaamini watakuwa waathirika katika mchakato huo.

Alisema mawakili wao wanawasilisha vifungu mbalimbali vya sheria, lakini wanaona havitiliwi maanani ikiwamo katika pingamizi la kwanza kuhusu mamlaka ya mahakama.

"Uamuzi uliotolewa haukutilia maanani kifungu namba 11 cha Sheria ya Ugaidi kilichowasilishwa na mawakili, hakikuzungumziwa kabisa katika uamuzi wakati ndicho kifungu kinachosisitiza mamlaka ya sheria, dhidi ya sheria yoyote panapotokea mgongano.

"Uamuzi wa leo, tumeendelea kuona kusahaulika ama kwa bahati mbaya au makusudi kwa baadhi ya hoja zinazowasilishwa na mawakili, tukiendelea hivi haki zetu za msingi katika shauri hili hazitapatikana.

"Ni ukweli usiopingika kwamba kesi hii inavuta hisia nyingi ndani ya jamii, itakuwa vyema hatua zote zitaonekana na zitabakia kuwa zimefanyika kwa haki na weledi bila hisia yoyote ya uonevu.

"Hisia mbalimbali za jamii katika suala hili inaweza kuthibitisha katika mijadala inayoendelea katika mitandao ya kijamii hatuwezi kupuuza," alidai Mbowe.

Alidai hawawezi kupuuza taarifa za Mtandao wa Weekleas na aliomba kunukuu kilichoandikwa katika Mtandao huo.

"Jaji Elinaza Luvanda ni mserikali na TISS, yuko Mahakama ya Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi kimkakati, ameelekezwa kumfunga Mbowe huku Msajili akishughulika na CHADEMA, Rais atamwachia baada ya muda, kila pingamizi atalitupilia mbali haijalishi uhalali wake," alinukuu Mbowe maneno hayo yaliyoandikwa mtandaoni.

Mbowe alidai maneno hayo hawawezi kuyapuuza katika kutoa haki na aliomba ikimpendeza Jaji Luvanda ajitoe kusikiliza shauri hilo, ili kujenga heshima yake, heshima ya mahakama, asibebeshwe lawama ambazo pengine hazikustahili.

Jaji Luvanda akijibu alisema msingi wa malalamiko ni dhana kuliko uhalisia, lakini hana sababu ya kujitetea kwa jambo ambalo halipo.

"Shauri lina maslahi mapana ya umma, naona ni busara nikae pembeni jaji mwingine aendelee nilipoishia.

"Niwashukuru wote kwa ushirikiano tangu mwanzo, nawaombea kila la heri inshallah, shauri linaahirishwa kusubiri jaji mwingine atakayepangiwa," alisema Jaji Luvanda.

Katika shauri hilo Jamhuri inawakilishwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Kidando, Katuga, Ignas Mwinuka, Esther Martin na Wakili wa Serikali Tilimanyo Magige. Upande wa utetezi unawakilishwa na Wakili Peter Kibatala, Jeremiah Mtobesya, John Mallya, Jebra Kambole, Frederick Kihwelo, Sisty Aloyce, Selemani Matauka, Nashon Mkungu, Michael Rugina, Bonifasia Makungu, Alex Maseba, Faraja Mangula, Michael Mwangasa na Gaston Shundu.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Halfan Bwire, Adam Kasekwa, maarufu Adamu na Mohamed Ling'wenya, ambao wanakabiliwa na mashtaka sita.

Katika shtaka la kwanza wanadaiwa wote, walikula njama kati ya Mei Mosi na Agosti Mosi 2020 katila Hoteli ya Aishi iliyopo Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro na maeneo mbalimbali ya jiji la Dar es Salaam, Morogoro na Arusha, kulipua vituo vya mafuta kuhatarisha usalama wa Taifa na kusababisha hofu kwa jamii.

Shtaka la pili wote wanadaiwa kula njama kufanya vitendo vya kigaidi na kutaka kumsababishia majeraha aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Sabaya.

Shtaka la tatu, Mbowe anadaiwa katika kipindi hicho na mahali hapo aliwawezesha kifedha Halfani, Adamu na Ling'wenya huku akiamini fedha hizo zitasaidia katika kufanya ugaidi


kwa kulipua vituo mbali mbali vya mafuta na mikusanyiko kwa lengo la kuharibu misingi ya kisiasa, katiba, uchumi na sifa ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Shtaka la nne wanadaiwa kushiriki vikao vya kufanya vitendo vya kigaidi.

Shtaka la tano, mshtakiwa Adamu anadaiwa Agosti 5 mwaka 2020 eneo la Rau alikutwa na bastora yenye namba A 5340 aina ya Luger.

Mshtakiwa Halfani katika shtaka la sita anadaiwa Agosti 10 mwaka 2020, kwa lengo la kuhatarisha usalama wa nchi alitumia sare za Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) na Jeshi la kujenga Taifa(JKT) ambazo ni suruali moja ya JKT, pamoja na suruali nne za JWTZ, fulana moja, Koti la mvua moja, jacket moja, kofia tano, overall tano, begi la kubebea vifaa vya JWTZ lijulikanalo kwa jina la ponjoo, vyeo vinne vya koplo, mikanda minne, soksi jozi moja, sweta, begi la mafunzo ya parachuti, kibuyu cha kunywea maji pamoja na kisu aina ya AK 47 CCCP, vyote vya JWTZ.

TANGAZO


NMB
FOUNDATION
Kuboresha Maisha ya Jamii ya Tanzania
Elimu
Afya
Kilimo
Mazingira
Ujasiriamali
Tunaposimama pamoja kukabili changamoto zetu, tunajenga na kukuza vyanzo endelevu vya kuimarisha uchumi na mstakabali mzima wa maisha yetu kama Taifa.
www.nmbbank.co.tz
nmbfoundation@nmbbank.co.tz

MAHOJIANO MAALUM

# Mkuu PAC: Kuna shida uteuzi mawaziri na watendaji wakuu

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

UNAPOMTAJA Naghenjwa Kaboyoka, unarejea jina la Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA) ambaye katika sura ya pili anakalia kiti kuongoza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC).

Ndani ya kofia hiyo na utashi binafsi, ana maoni kadhaa anayoamini mambo hayajakaa vizuri katika maeneo ya kimfumo serikalini ikiwamo uteuzi wa mawaziri, watendaji wakuu wa taasisi za umma na utekelezaji maoni rasmi ya kitaalamu kuboresha mwenendo huo.

Ni kwa vipi? Ili kupata undani wake, Nipashe imepata faragha na Mwenyekiti wa PAC huyo na ifuatayo ni sehemu ya mazungumzo ya kina ya maswali na majibu:

---

**SWALI:** Ukipata muda wa kuteta na Rais Samia leo, utamshauri jambo gani muhimu kwa taifa?

**KABOYOKA:** Jambo la kwanza ambalo nitamshauri; haya mashirika ya umma, viongozi wake wasiteuliwe na Rais, waombe zile kazi na kuwe na kamati ambazo zinawachukua na kuwafanyia tathmini kuona kwamba 'huyu ana utaalamu unaotakiwa'.

Ukimshamteua unamfanya kwamba awe anakusikiliza wewe. Kama ni kiongozi ambaye aliomba ile kazi na ameshindwa kuifanya ipasavyo, inakuwa rahisi kumfukuza. Kwa utaratibu wa sasa hata mkuu mwenyewe anapata kigugumizi 'sasa nitafukuza wangapi?'

Kwa hiyo, jambo la kwanza ambalo litamshauri, mashirika yetu haya yanayozalisha zile nafasi za viongozi wake zitangazwe, asichukuliwe mtu akawekwa pale kwa uteuzi.

Lengo ni kwamba wale wanaomfanyia usaili na yule anayefanyiwa usaili ajue anaahidi anatafanya A, B, C, na hivyo vigezo atawajibika navyo. Asipotimiza, basi wanaeleza tu kwamba huyu mtu atolewe. Hilo ni la kwanza.

La pili; Kama kuna nafasi ya kurekebisha sheria, mawaziri wasitokane na wabunge. Ni kwa sababu huyo waziri anayeteuliwa huku akiwa mbunge, ana maslahi yake fulani. Matokeo yake hawezi kuwa impartial (kutokuwa na upendeleo).

Anajigawanyaje? Ndio maana utakuta huku kunaenda maendeleo sana kwingine haukuendi. Hilo ni gumu lakini ndio linaharibu kazi.

Kwa hiyo, ni vigumu sana kufukuzwa fukuzwa au kuachishwa na kusemwa maana kule kuna ule 'uchama', mtu anasema 'aah huyu ni mwenzetu, tunyamaze'. Tunasifu tu, yaani anasifiwa hata pale ambapo anafanya vibaya.

Lakini kusema 'hapana, huyu tumtoe, Bunge hatumtaki huyu waziri hafanya kazi ipasavyo' inakuwa ngumu.

Kwa hiyo, tuna vitu ambavyo kwa kweli vinahitaji Rais atusaidie. Ninajua hili litakuwa gumu, lakini hilo la mashirika kwamba kazi zitatangazwe ninaamini liko kwenye uwezo wa Rais.

Hawa CEOs wa mashirika yetu kazi zitangazwe na hao wakurugenzi wa hizo bodi wawe watu wanaoweza kazi. Siyo mtu ametoka tu chuo kikuu anaambiwa akakae pale. Ndio maana bodi nyingi unakuta hazifanyi vizuri.

**SWALI:** Ni kwa kiasi gani mapendekezo ya PAC yanafanyiwa kazi na serikali?



Mwenyekiti wa PAC, Naghenjwa Kaboyoka.

**KABOYOKA:** Kwa kweli hatujafanya tathamini lakini ukiangalia marudio ya masuala yale yale yanayotokana na Ripoti ya CAG (Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali), yanakwambia kwa kiasi gani mapendekezo yetu hayajafanyiwa kazi.

Kwa mfano, Mamlaka ya Bandari (TPA) tumezungumza mifumo leo ni mwaka wa tano haijarekebishwa.

Na unakuta kuna mtu ameajiriwa pale kwa consultant wa hiyo mifumo na inafeli mmoja baada ya mwingine, yupo tu na anaendelea kulipwa. Unajiuliza 'kwa nini tunatoa hizi ripoti na habadilishwi?'

Kwa hiyo, mimi ninasema mapendekezo yetu kwenye yale mashirika makubwa bado hayajafanyiwa kazi. Na haya ndio tunayategemea yatuletee hela.

Bandari ni sehemu kubwa ambayo ingetuletea hela nyingi sana, lakini mifumo haisomani. Na kama haisomani, ni rahisi fedha kuvuja kienyeji tu bila kujulikana imeenda wapi na imetoka wapi.

Na sisi PAC tunapeleka mapendekezo na yanapitishwa kama maazimio ya Bunge lakini sijaona Bunge likisema sasa hawa wafukuzwe kazi.

Wale ambao wanafanya vibaya, mfano Wizara ya Maji, unafikiria bajeti yao isipitishwe na Bunge lakini inakuwa 'hapana, wananchi watapata tabu'.

Fedha ya miradi ya maji inapelekwa lakini miradi haitoi maji na fedha nyingi zimetumika. Sasa hapo umesaidia nini? Umeisaidia hiyo wizara? Kwa hiyo, mfumo wetu wote ni mbaya, ni mbaya!

Bunge tunaishauri serikali na tunaisimamia, lakini hatuna nafasi ya kusema 'sasa hapana, waziri ajiuzulu'. Yule aliyemweka ndiye mwenye usemi. Kwa hiyo, mimi ninasema kwamba bado tuna kazi kubwa.

**SWALI:** Mwalimu Nyerere alikuja na kitu kinachoitwa SCOPO. Kwa hali inayoendelea kwenye mashirika ya umma nchini, unafikiri SCOPO irejeshwe?

**KABOYOKA:** Unajua unaposema unafanya biashara huria na mtu wako unataka afanye biashara, hapo ndipo tatizo linapokuwapo.

Mkuu wa shirika la umma ambapo kawaida unakuta yule kiongozi wake, yaani CEO (Ofisa Mtendaji Mkuu) anateuliwa, hapatakuwa na ushindani. Maana kukiwa na ushindani, unasema 'mimi hili shirika litaliendesha na litahakikisha linafanyaje kazi?'

Leo CEO unateuliwa na kiongozi halafu kiongozi huyo huyo atakwambia 'hapa ninahitaji Sh. bilioni mbili, leta'. Namna gani? 'Wewe fanya uwezavyo'. Je, unaweza kukataa, huwezi.

Kwa hiyo utaratibu wa hasara unaanzia hapo, hata ukirudisha SCOPO, haitasaidia. Ingekuwa mashirika haya yanafanya ushindani, viongozi wake wakachukuliwa kwa uwezo wao, sio kwa kigezo cha uanachama kindakindaki, tungepiga hatua kubwa.

Kwa hiyo, shida sio mfumo, shida iko kwenye uteuzi wa hao wanaosimamia mashirika ya umma. Inatakiwa sasa viongozi wetu waone mashirika haya yanafanya kazi kibiashara inavyotakiwa.

Wewe kiongozi unaniambia nikuletee hiyo fedha, kesho utanizuiaje kwenda kufanyia mkutano nje ya nchi? Unachukua wafanyabiashara wengi kwenda Marekani kutafuta biashara, wakirudi hakuna hata mmoja aliyerudi na biashara yoyote. Wametumbua hela ya serikali.

Kesho na sisi tukisema tunataka kwenda Dubai kufanya mkutano wetu wa mwaka utatukatazaje? Kwa hiyo, tatizo lipo hapa kwenye viongozi wa kuteuliwa teuliwa. Hakuna ushindani.

Sisi hapa unakuta hata bodi yenyewe ya shirika ni CEO tu ndio anajua uendeshaji wa shirika. Hao wengine wamechukuliwa tu kwa sababu huyu ni profesa. Profesa wa hesabu chuo kikuu unampelekaje kwenye shirika? Nadharia na vitendo ni vitu viwili tofauti.

Watu wengi wana elimu ya nadharia, unakuta amekuwa mhadhiri chuo kikuu kwa miaka nenda rudi, ndiyo maana hata wahadhiri wa chuo kikuu leo ukimwambia akafanye biashara hawezi, anafilisika.

***ITAENDELEA KESHO**

HABARI KITAIFA

## MAT yalaani mgonjwa kufumuliwa nyuzi

**Na Christina Mwakangale**

CHAMA cha Madaktari Tanzania (MAT) kimelaani vikali kitendo kilichofanywa na daktari wa Kituo cha Afya Kerege wilayani Korogwe mkoani Tanga, Jackson Meli, kufumua nyuzi kwenye jeraha la mgonjwa, kikisema ni kinyume na maadili ya taaluma ya kitabibu.

Kimesema maadili ya taaluma yanaagiza daktari kutokuwa sehemu ya kusababisha madhara kwa mgonjwa kwa namna yoyote ile.

Tamko lililotolewa jana na Rais wa chama hicho, Dk. Shadrack Mwaibambe, lilieleza kuwa hatua za kisheria zifanyike ikiwamo kumfikisha mtuhumiwa wa tukio hilo katika baraza la kitaaluma.

"Tunapongeza mamlaka husika kwa kuchukua hatua stahiki za awali kwa mtuhumiwa na tunaomba utaratibu wa kisheria uchukue mkondo wake ikiwa pamoja na kufikishwa kwenye baraza la kitaaluma.

"Wanataaluma na hospitali zote zinakumbushwa kufuata utaratibu wa EMTALA 1986 ambao Tanzania imeridhia na inautekeleza. Mgonjwa yoyote katika hali ya dharura ana haki ya kupewa huduma ya kwanza katika hospitali yoyote iliyokaribu bila kujali ni ya binafsi au ya serikali," alisema Dk. Mwaibambe.

Alisema huduma kwa mgonjwa yoyote hutolewa bila kujali anauwezo wa kulipia huduma au hana, kwamba sharti hilo limeridhiwa na hospitali zote kabla ya kupewa usajili.

Alibainisha kwa kutoa wito kuwahusu madaktari kwamba kuna umuhimu wa kuhudhuria mikutano ya kitaaluma ya kukumbusha maadili ya udaktari na kuongeza ufanisi wa utoaji huduma kwa wagonjwa.

# IGP, vyama vya siasa uso kwa uso

**Na Elizabeth Zaya**

OFISI ya Msajili wa vyama vya siasa, vyama vya siasa na Jeshi la Polisi likiongozwa na Mkuu wa Jeshi hilo (IGP), Simon Sirro, vinatarajia kukutana katika mkutano wa maridhiano na kuweka sawa namna ya kuendesha shughuli za kisiasa nchini bila kukwaruzana.

Msajili wa vyama hivyo, Jaji Francis Mutungi, akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana, alisema wakati wakisubiri kufanyika kikao hicho, hatarajii kuona vyama vya siasa vikiandaa kufanya mikutano na makongamano kabla ya mkutano huo.

Alisema lengo la mkutano huo ambao hakuweka wazi tarehe ya kufanyika kwake, ni pamoja na kujadili namna ya kuondoa kile kinachoonekana kwamba upo uhasama kati ya Jeshi la Polisi na vyama vya siasa pamoja na namna ya kuweka vizuri utaratibu wa kuendesha mikutano ya kisiasa.

"Nimewaita leo, ili kuwaeleza kuwa tunatarajia kufanya mkutano wa kuondosha mvutano unaojitokea kati ya polisi na vyama vya siasa, yawezekana umma ukafikiri kwamba tumekalia kimya hilo suala, nikaona ni busara niwaite ili kuuhabarisha kwamba hatujakalia kimya hii hali ambayo inaonekana kama inaleta taharuki fulani,"alisema Jaji Mutungi.

"Msajili kama mlezi wa vyama na msimamizi wa sheria ya vyama hivyo, niliwasiliana na IGP na tukakubaliana kimsingi, tuwaite wadau hawa kwenye suala hili, katika kikao hicho, tunataka kuwaita polisi wakiongozwa na IGP mwenyewe, Ofisi ya Msajili na viongozi wakuu wa kitaifa wa vyama vyenye usajili wa kudumu, lengo ni kukaa chini, kuwa na maongezi kuhusiana na suala hili hususani mikutano ya ndani, makongamano na kadhalika."

Jaji Mutungi alisema mvutano kati ya vyama hivyo na Jeshi la Polisi, limeanza kujenga taswira hasi kwa umma.

"Tumeacha imekuwa kama inajenga taswira ambayo ni hasi kwa umma, tusingependa pia ifike mahala watu waanze kuogopa, kila mkutano wa siasa, mapolisi wamejaa, kila shughuli ya wanasiasa mapolisi wamejaa, this is not a military state, naamini katika mkutano huo tutatoka na mwelekeo mzuri na wenye tija kwa taifa hili," alisema Jaji Mutungi.

"Sisi kama Ofisi ya Msajili, tunawiwa kuutarifu umma kuwa siasa ya nchi yetu haijafikia hatua hiyo ya taharuki zisizo na mbele wala nyuma, na pia nisingependa kutumia neno ambalo wengi wamezoea kulitumia, sintofahamu. Sisi tunasema hakuna sintofahamu, ni suala tu la kuwekana wazi na kueleweshana."

"Na tunapozungumza na familia ya wanasiasa ni watu wazima na ni wenye uchungu na nchi. Tunataka tuondoshe hicho kitu ambacho polisi wanaona kwamba labda wanasiasa wanakosea, na wanasiasa nao wanaona polisi wanakosea hapa, hivi kwa nini tusikae meza moja tukaweka bayana wapi tunapishana."

Aliwaomba vyama vya siasa kuwa subira ya kutofanya mikutano na makongamano yoyote katika kipindi hiki wanachosubiri kufanyika mkutano huo.

Baaadhi ya wadau wa vyama hivyo wamepokea kwa kauli tofauti kuhusu kuitishwa kwa mkutano huo, baadhi yao wakisema hawako tayari kushiriki kabisa mkutano huo, na wengine wakisema watashiriki lakini hawako tayari kuacha kufanya mikutano na makongamano ya ndani kwa kusubiri tukio hilo.

Kwa upande wa NCCR-Mageuzi, wao walisema hawako tayari kushiriki kwenye mkutano huo na kwamba mkutano pekee ambao wanataka ufanyike wa kuhusisha vyama hivyo ni wa Rais Samia Suluhu vyama hivyo au Waziri wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene.

Naibu Katibu wa Habari, Uenezi na Mawasiliano ya Umma, wa Chama cha ACT-Wazalendo, Janeth Ritte, alisema chama chake kitajadili endapo kitashiriki au laa mkutano huo, lakini mikutano ni vigumu kusitisha kwa sababu mipango cha chama lazima iendelee.

Naibu Katibu Mkuu Bara wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Benson Kigaila, alisema kuhusu kushiriki kwenye mkutano huo chama hicho kitajadili lakini hawako tayari kusitisha mikutano kusubiri kwa sababu ni haki yao kufanya mikutano hiyo.

Mkurugenzi wa Habari, Mawasiliano ya Umma na Itikadi wa Chama cha Wananchi (CUF), Mohamed Ngulangwa, alisema chama chao kimepongeza hatua ya Msajili kuitisha mkutano huo isipokuwa kimesikitishwa na kauli yake ya kuviomba kuzuia kwa muda mikutano hadi mkutano huo ufanyike.

# PM: Taasisi za serikali toeni huduma pamoja

**Na Romana Mallya**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameziagiza taasisi za serikali ambazo hazijaanza kutoa huduma kupitia vituo vya Huduma Pamoja vya Shirika la Posta Tanzania zihakikishe zinaanza kutoa huduma katika vituo hivyo ndani ya mwaka huu wa fedha.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati wa uzinduzi wa Vituo vya Huduma Pamoja inayotolewa katika ofisi za shirika hilo ambapo kwa kuanzia imeanza na Dar es Salaam na Dodoma na hadi ifikapo 2025 zitakuwa zimeenea nchi nzima.

Baadhi ya huduma zinazotolewa ni pamoja na za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Wakala wa Vizazi na Vifo (RITA), Idara ya Uhamiaji, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), halmashauri za majiji na huduma za kifedha inayotolewa na CRDB.

Alitaja baadhi ya taasisi ambazo bado hazijaanza kutoa huduma katika vituo hivyo kuwa ni Tume ya Ajira, Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA), Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Maeneo Maalumu ya Uwekezaji kwa Mauzo ya Nje (EPZA) na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

Majaliwa alisema Rais Samia Suluhu Hassan hataki kuona wananchi wanapata tabu ya kupata huduma na kutaja maelekezo mahususi kwa kila sekta zilizojiunga na huduma hiyo na ambazo bado.

Aliitaka Wizara ya Mawasiliano Teknolojia ya Habari ambayo ndiyo msimamizi wa mradi huo iongeze kasi ya utekelezaji ili kuhakikisha matatizo ya wananchi ya kupata huduma zinatatuliwa.

"Pili, wizara hii mhamasishe mnakuwa na ubunifu wa utafiti katika Shirika la Posta ili kuleta mapinduzi ya bidhaa. Tatu, Ofisi ya Rais, Menejimenti na Utawala Bora hakikisheni taasisi zote zinazotoa huduma za serikali zinazitoa katika vituo vyote vya huduma pamoja ifikapo mwaka 2022," aliagiza.

Pia alitaja jambo la nne ni wizara zinazosimamia taasisi zinazotoa huduma mbalimbali kwa wananchi mfano afya na elimu zizielekeze zile zilizopo chini yao zianze kutoa huduma katika vituo hivyo.

"Tano, Shirika la Posta Tanzania hakikisheni mnatumia fursa hii vizuri andaeni majengo, simamieni huduma ziwe za weledi, ziepuke kuwa na malalamiko pia tuwe na wapokeaji wakarimu kwenye dirisha la mapokezi watakaotoa maelekezo thabiti, moja ya eneo ambalo mnapaswa kuliimarisha ni huduma za ukarimu, alisema.

Alitaja jambo la mwisho ni taasisi zote zinazotoa huduma kwa wananchi ziache urasimu na kuhakikisha ndani ya mwaka huu wa fedha huduma hizo zinatolewa.


## MCHUANO TUZO ZA ICT 2021 WAPAMBA MOTO

Katika kutambua mchango wa watu binafsi, taasisi na makampuni katika matumizi ya teknolojia, Tume ya Tehama Tanzania (ICT Commission) imeandaa tuzo maalum zenye vipengele 20.

Zoezi hilo la utoaji tuzo limezinduliwa Agosti 25, 2021 na Mkurugenzi Tume ya Tehama, Samson Mwela, na kusisitiza kuwa wananchi wenyewe watapendekeza washiriki kupitia tovuti ya tume https://www.ictc.go.tz/

"Tuzo hizi tumeziweka kwenye makundi mbalimbali, moja ya makundi hayo ni eneo la Ubunifu, ambapo hapa tutatambua kampuni bora changa ya Tehama, pia tutakuwa na Atamizi bora, ambapo hizi kwenye tehama ni zile zinasazosaidia huduma mbalimbali kufika kwa jamii na nyingine ni wanafunzi wabunifu kwenye tehama hapa ni wa kike na wa kiume wote tutawatambua", aliesema Mwela.

Hivi sasa zoezi linaendelea kwa watu kupendekeza washiriki hadi Septemba 11 na baada ya hapo, tume itatoa nafasi kwa walipendekezwa kujaza fomu hadi Septemba 18 kwaajili ya hatua inayofuata.

Utaratibu wa kupendekeza ni kuingia tovuti ya ictawards.ictc.go.tz kisha kujaza jina la mtu unayefahamu ni mbunifu wa tehama.



Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Tehama Tanzania (ICT Commission ) Samson Mwela akifafanua jambo wa Timu ya East AFrica TV na Radio, kuhusu Tuzo za Tehama ( ICT Awards 2021 )

**Vipengele Vinavyowaniwa – ICT Awards**

1. Best Ict Startup (Kampuni Changa Bora ya Tehama)
2. Best Ict Incubation Hub (Atamizi Bora ya Tehama)
3. Best Innovative Ict Student (Female) (Mwanafunzi Mbunifu Bora wa Tehama wa Kike)
4. Best Innovative Ict Student (Male) Mwanafunzi Mbunifu Bora wa Tehama wa Kiume
5. Best Mobile Network Operator (Kampuni Ya Mawasiliano Iliyotoa Huduma Bora Kwa Jamii (Csr)
6. Best Company Providing Services On It (Kampuni Inayotoa Huduma za Tehama (Outsource) Bora)
7. Best Company In Software Development (Kampuni Bora Katika Kutengeneza Mifumo ya Tehama)
8. Best Ict Transformative Training Institution (Taasisi Ya Mafunzo Bora Kwenye Kutumia Tehama)
9 Best Institution In Provision Of Health Services Using Ict (Taasisi Bora Inaotumia Tehama Katika Utoaji wa Huduma za Afya)
10. Best Financial Institution In Using Ict (Taasisi ya Kifedha Bora Katika Kutumia Tehama
11. Best Financial Technology Company (Kampuni Bora ya Teknolojia Ya Fedha
12. Best Female Ict Researcher (Mtafiti Tehama wa Kike Bora)
13. Best Male Ict Researcher (Mtafiti Tehama wa Kiume Bora
14. Best Company In Digital Insurance Services (Kampuni Bora Katika Huduma za Bima Kidijitali
15 Best Lga In Using Ict Applications (Halmashauri Bora Inayotumia Tehama Kutoa Huduma Kwa Jamii)
16. Best Ict Solution In Agriculture (Mfumo Wa Tehama Bora Katika Kilimo
17. Best Artist In Using Icts For Development (Msanii Bora Anayetumia Tehama/Mitandao Vizuri)
18 Best Jounalist In Using Ict For Development (Mwandishi wa Habari Bora Anayetumia Tehama/ Mitandao
19. Best Media House In Using Ict For Development (Chombo Cha Habari Kinachotumia Tehama)
20. Best Ministry On Ict Integration In Sectors Policies Award (Wizara Bora Katika Ujumuishaji Wa Tehama Kwenye Sekta Za Uchumi).


Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Tehama Tanzania (ICT Commission ) Samson Mwela kwenye picha ya pamoja na Wanahabari na Watangazaji wa East Africa Television na East Africa Radio baada ya mafunzo aliyowapatia ofisini kwake kuhusu Tuzo za Tehama ( ICT Awards 2021 ) na Mkutano Mkuu wa Tehama utakaofanyika Arusha 20-22 Oktoba 2021.

Nipashe
MWANGA WA JAMII




## Filamu inayomshirikisha Rais suluhisho bora utata tanzanite

**TANZANIA** ina neema ya utajiri wa aina nyingi, kuanzia madini ya vito vya thamani kama dhahabu, almasi hadi tanzanite, isiyopatikana kwingine kokote duniani.

Usafirishaji na uuzaji wa tanzanite unaofanywa na baadhi ya majirani wa Tanzania na baadhi ya nchi za mbali zikiwamo kutoka Bara la Asia, umekuwa ukiendana na upotoshaji dunia, hata baadhi wakaamini madini hayo si ya nchi hii.

Hali hiyo kwa namna moja au nyingine, imesababisha nchi kukosa fedha za kigeni ambazo zingetokana na uuzaji wa madini hayo sehemu mbalimbali duniani, hasa ikizingatiwa ukweli kwamba yana thamani kubwa.

Kutokana na hali hiyo, Rais Samia Suluhu Hassan, ameshajitoa kimasomaso kuchukua hatua ambazo huenda zitamaliza utata wa upotoshaji huo wa muda mrefu, kuhusu tanzanite, kwamba isijulikane kuwa inapatikana kwa upekee nchini Tanzania.

Anachokifanya Rais Samia kwa sasa, ni kushiriki utengenezaji filamu itakayoonyesha mazuri yaliyopo nchini. Alishaanza kwenye mgodi wa Mirerani, wilayani Simanjiro mwishoni mwa wiki iliyopita, akinuia kuionyesha dunia tanzanite ni ya Tanzania, kama jina lake linavyoashiria.

Yeye na timu yake wamekwenda kwenye machimbo, wanachukua picha namna madini yanavyochimbwa, inavyopimwa, inavyoongezwa thamani hadi pale vinapopatikana vito vya madini hayo.

Kwa mujibu wa Rais, sasa wale wanaouza ovyo huko nje ya nchi, wajue kuwa ni madini yatokayo Tanzania na kwamba hata dunia nayo ithamini uhalisia ulioko, kwa kuwa yeye na timu yake wanaonyesha ilivyo.

Tunaamini kuwa hatua hiyo ya serikali itaisaidia dunia kujua ukweli kuhusu sehemu yanakotoka madini hayo, kuliko ambavyo imekuwa ikielezwa na baadhi ya wapotoshaji kimataifa kwamba tanzanite haitoki kwetu.

Kimsingi, Tanzania ina vivutio vingi vikiwamo mbuga za wanyama ambazo watalii hupenda kuzitembelea na sasa Rais Samia ameamua kujitosa kimasomaso kutangaza vivutio vyote vya nchi hii kupitia filamu. Ni uamuzi unaopaswa kupigiwa makofi na kila mtu.

Jamii sasa inaona kuwa ni wakati mwafaka wa dunia kujua Tanzania ilivyo kuanzia utajiri wake wa madini, hadi vivutio vilivyomo, ili watalii waje kwa wingi na kuifanya nchi ipatwe fedha nyingi za kigeni kwa ajili ya maendeleo yake.

Ni matarajio yetu kwamba uandaaji filamu hiyo, pia utasaidia kuondoa utata wa muda mrefu kuhusu ulipo Mlima Kilimanjaro ambao baadhi ya watu nje ya nchi wanadhani haupo Tanzania.

Hiyo inatokana na ukweli kwamba, baadhi ya watu walioko mbali wamekuwa wakiamini mlima huo upo katika nchi jirani hata kuinyima nchi watalii, hali inayosemekana ni zao la baadhi ya zinazolazimisha kuchangamkia fursa zisizo za kwao.

Hatua ya kutengeneza filamu hiyo, tunaichukulia kama suluhisho la utata ambao umekuwapo muda mrefu hasa kwenye madini ya tanzanite, hali kadhalika Mlima Kilimanjaro, ukipotoshwa sio mali ya Tanzania.

Kwa mwendo huo, tunaona wazi sasa dunia itajua ukweli jinsi Tanzania ilivyo na utajiri wa madini ya kipekee, pia vivutio vya asili hata wawekezaji kuja nchini kwa ajili ya miradi mbalimbali kama ya uchimbaji, hata kushuhudia vivutio vya kitalii.

Hivyo, wito wetu ni kuwataka Watanzania kuunga mkono juhudi hizo za Rais Samia kwa lengo la kujipatia fedha nyingi za kigeni, kwa kutumia madini na vivutio vilivyopo kunufaisha maendeleo ya nchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



### Muungwana Lazima Nilonge

## Mbinu hizi ni muhimu kukuza vipaji vya wanafunzi

Na Sabato Kasika

**SABABU** mojawapo ya wazazi na walezi kupeleka watoto wao shule ni kutaka wapate elimu, ujuzi na stadi mbalimbali na kwa kuanza wawe na uwezo wa kujua kusoma, kuandika na kuhesabu, kutokana na kwamba hatua hiyo ni ya umuhimu katika maisha.

Kujifunza katika muktadha huo, kunawahitaji watoto kufanya mazoezi ya namna mbalimbali za kutengeneza taarifa na kuendeleza uwezo wa kuchagua tabia ambazo watu wazima wanatarajia watoto waliosoma kuwa nazo.

Shule zinazoheshimu na kujali vipaji vya wanafunzi, huwa mstari wa mbele kuibua na kuviendeleza kwa lengo la kupata wataalamu wa fani mbalimbali wa baadaye watakaokuwa na mchango kwa taifa lao.

Hizo kwa wataalamu wa elimu, kwa ujumla wake wanaziita stadi za utambuzi, kwa lengo la kubaini wale wenye uwezo wa kubuni vitu na kuwatia moyo waendelee kuchukua hatua za kuhakikisha wanasonga mbele.

Miongoni mwake ni ubunifu na ugunduzi ambavyo ni nguzo kwa taifa linalotaka kukua kisayansi na kiteknolojia, na kwa mataifa ambayo yanatambua umuhimu huo, yanapobaini vipaji na ubunifu, huviendeleza.

Hayo hufanyika kutokana na kwamba, ubunifu ndilo eneo sahihi la kuwekeza kwa ajili ya maendeleo endelevu ya watu wa nchi husika badala ya kutegemea vipaji, ubunifu na ugunduzi kutoka kwingine.

Kwa kawaida, mwanafunzi anayejitambua hategemei anachofundishwa na mwalimu pekee, bali kujiongeza kwa kuwa mbunifu, kwani kwenye ulimwengu huu wa sayansi na teknolojia, ubunifu ni muhimu.

Umuhimu wake ni kwamba unaweza kumsaidia katika soko la ajira pindi anapohitimu, ndivyo wanavyofanya wanafunzi wa Shule ya Msingi Genesis ya jijini Dar es Salaam.

Pamoja na umri wao mdogo wa miaka kati ya tisa na 10, vichwani wako vizuri kutokana na kubuni vitu mbalimbali ikiwamo roboti ya kunyanyua mizigo, sola na vitu vingine ambavyo vinaonyesha jinsi walivyo wabunifu.

Wanafunzi wa shule hiyo wenye ndoto ya kuja kuwa wataalamu wa fani mbalimbali wa baadaye ni wazi kwamba, ubunifu wao unaweza kutajwa kama kielelezo cha umuhimu wa kuibua vipaji.

Meneja wa shule hii, Joachim Jovin anasema, katika kuibua vipaji vya watoto, shule imekuwa ikishirikisha wazazi na walezi kwa kuwaelekeza kutambua vipaji vya watoto wao na kusaidia kuviendeleza.

Kwa mujibu wa meneja huyo, kila mwaka shule hiyo imekuwa ikiandaa maonyesho maalum yaitwayo 'Siku ya Mradi wa Sayansi' kwa lengo la kuona kipaji cha kila mwanafunzi.

Katika maonyesho hayo, kila mwanafunzi hujitahidi kuonyesha kile ambacho anaweza kukitengeneza au kubuni na kisha kazi ya mwalimu huwa ni kusaidia kuendeleza kipaji cha mwanafunzi kulingana na ubunifu.

Hatua zinazochukuliwa na shule kwa wanafunzi wake, ni kama zinalenga kurejesha wazo la Mwalimu Nyerere la elimu ya kujitegemea, kwa kuibua vipaji, ili viweze kuwasaidia katika maisha yao ya baadaye.

Mwanafunzi wa miaka tisa au 10 kuonyesha uwezo wa kutengeneza sola, satellite au roboti yoyote, ni wazi kwamba akiendelezwa anaweza mtaalumu mzuri wa baadaye katika fani mbalimbali.

Hivyo, kuibua vipaji vya watoto wangali wadogo na kuviendelea, inaweza kuwa njia nzuri ambayo itafanya waweze kuwa wabunifu wa kubwa wa baadaye, kwa ajili ya maendeleo ya taifa lao.

Ni kweli kwamba vitu vingi ambavyo watoto wamekuwa wakivitengeneza, ni vile ambavyo vilishabuniwa au kuvumbuliwa na watu wengine karne nyingi zilizopita, lakini wakiendelezwa, inawezekana nao wakabuni vya kwao.

Lakini kwa umri wao mdogo walionao na wakaweza kujaribu kuiga vile ambavyo vilishatengenezwa na wengine, ni hatua kubwa ambayo inaonyesha ni jinsi gani walivyo na vipaji vya kuweza kufanya vitu vikubwa baadaye.

Wakifikia hatua kama hiyo wakiwa watu wazima wanaweza kujiajiri na hata kuajiri wengine na hivyo kusaidia serikali kukabiliana na uhaba wa ajira nchini, ambao unasababisha wasomi wengine kukaa bila kazi wakisubiri kuajiriwa.

Ninaamini kwamba, ubunifu kwenye teknolojia ukiongezeka, ukosefu wa ajira unaweza kupungua, kwani vijana watajiajiri na hata kuajiri wengine kulingana na taaluma walizonazo.

TANGAZO

SAMSUNG

Galaxy Z Fold 3 | Flip 3 5G

Kuwa wa kwanza

kupre-order

na upate zawadi za uzinduzi




Image simulated.
SPen Fold edition sold separately and is only compatible with Z Fold3 5G.

Pata GB96 BURE! Mwaka mzima

Nunua Galaxy Z Flip 3 (256GB)
Tsh 2,450,000
na upate Wireless Charger Duo + Leather Cover

Nunua Galaxy Z Fold 3 (512GB)
Tsh 4,440,000
na upate Wireless Charger Duo + Flip Cover with S Pen

216445202

4G+ 24 MONTH WARRANTY FOR AFRICA

Official partner
tigo

Ofa hii ipo mpaka Septemba 20. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tigo.co.tz
*Vigezo na masharti kuzingatiwa

# TANGAZO

## THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
## PRESIDENT'S OFFICE-REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
## BUKOMBE DISTRICT COUNCIL

# FINANCIAL STATEMENTS FOR THE YEAR 2019/2020

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

PRESIDENT'S OFFICE - REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

BUKOMBE DISTRICT COUNCIL

**STATEMENT OF FINANCIAL POSITION**

AS AT 30TH JUNE 2020.

| | Notes | 2020 TZS (000) | RE STATED FIGURE 2019 TZS (000) |
|---|---|---|---|
| **ASSETS** | | | |
| **Current assets** | | | |
| Cash and cash equivalents | 19 | 2,031,203 | 846,734 |
| Receivables and prepayments | 20 | 467,765 | 204,920 |
| Inventories | 21 | 335,663 | 466,098 |
| | | 2,834,632 | 1,517,752 |
| **Sub Total** | | 2,834,632 | 1,517,752 |
| **Non-current assets** | | | |
| Property, plant and equipment | 22 | 26,492,984 | 28,484,414 |
| Other financial assets | 24 | 41,316 | 41,316 |
| | | 26,534,300 | 28,525,730 |
| **TOTAL ASSETS** | | 29,368,932 | 30,043,482 |
| **LIABILITIES** | | | |
| **Current liabilities** | | | |
| Payables | 25 | 587,453 | 816,266 |
| Interest payable on loan | 27 | 224,681 | 3,055 |
| Employee benefits | 26 | 1,812,506 | 1,364,733 |
| Deferred income recurrent grant | 10 | 162,252 | 442,024 |
| | | 2,786,892 | 2,626,078 |
| **Non-current liabilities** | | | |
| Long term Borrowing | 27 | 867,920 | 1,069,163 |
| Deferred income capital grant | 28 | 1,598,619 | 177,104 |
| | | 2,466,539 | 1,246,267 |
| **TOTAL LIABILITIES** | | 5,253,431 | 3,872,345 |
| **NET ASSETS** | | 24,115,501 | 26,171,137 |
| Accumulated Surplus | | 24,074,185 | 26,129,821 |
| Minimum Compulsory Reserve | | 41,316 | 41,316 |
| **TOTAL NET ASSETS** | | 24,115,501 | 26,171,137 |

The financial statements were signed on behalf by:

Leah G. Kibaki
CMT Secretary
Date: 13/3/2021

Dionis M. Myinga
CMT Chairperson
Date: 13/3/2021

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

PRESIDENT'S OFFICE - REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

BUKOMBE DISTRICT COUNCIL

**STATEMENT OF FINANCIAL PERFORMANCE**

FOR THE YEAR ENDED 30TH JUNE 2020.

| | Notes | 2020 TZS ('000) | RE STATED FIGURE 2019 TZS ('000) |
|---|---|---|---|
| **Revenue** | | | |
| Local taxes | 9 | 687,526 | 442,256 |
| Amortisation of Recurrent grants | 10 | 24,428,103 | 23,210,968 |
| Fees, fines, penalties and licenses | 11 | 1,325,238 | 1,728,320 |
| Revenue from exchange transactions | 12 | 168,660 | 175,428 |
| Other own revenue | 13 | 7,263 | 27,298 |
| Amortisation of capital grant | 28 | 783,511 | 1,943,945 |
| | | 27,400,301 | 27,528,215 |
| **Expenses** | | | |
| Wages, salaries and employee benefits | 14 | 22,105,225 | 21,227,737 |
| Supplies and consumables used | 15 | 4,110,905 | 4,057,706 |
| Maintenance expenses | 16 | 670,470 | 439,487 |
| Finance costs | 17 | 101,881 | 195,042 |
| Provision for unbanked revenue | 20 | 48,160 | - 62,467 |
| Depreciation of property, plant and equipment | 22 | 1,548,681 | 2,173,538 |
| | | 28,585,321 | 28,031,043 |
| **deficit during the year** | | - 1,185,020 | - 502,828 |

The financial statements were signed on behalf by:

Leah G. Kibaki
CMT Secretary
Date: 13/3/2021

Dionis M. Myinga
CMT Chairperson
Date: 13/3/2021

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

PRESIDENT'S OFFICE - REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

BUKOMBE DISTRICT COUNCIL

**CASH FLOW STATEMENT**
**FOR THE YEAR ENDED 30TH JUNE 2020.**

| | NOTE | 2020 ('000) | RE STATED FIGURE 2019 ('000) |
|---|---|---|---|
| **Cash flows from operating activities** | | | |
| **Receipts** | | | |
| Taxes and levies | 9 | 688,254 | 416,798 |
| Fees, fines, penalties and licenses | 11 | 1,340,255 | 1,693,311 |
| Revenue From Exchange Transactions | 12 | 170,660 | 173,426 |
| Recurrent grant Received for year | 10 | 23,768,522 | 22,688,857 |
| Capital Grant Received | 38 | 2,187,826 | 1,564,539 |
| Other income | 13 | 3,825 | 27,298 |
| Receipts for Deposit Account | 40 | 1,025,565 | 805,404 |
| **Payments** | | | |
| Employee costs | 14 | - 21,657,452 | - 21,304,894 |
| Payments to suppliers | 15 | - 3,668,367 | - 3,442,284 |
| Maintenance expenses | 16 | - 623,977 | - 371,024 |
| Re payment of Loan | 27 | - 20,999 | - 17,856 |
| Payments for Deposit Account | 40 | - 958,060 | - 583,596 |
| **Net cash from operating activities** | | 2,256,053 | 1,649,980 |
| **Cash flows from investing activities** | | | |
| Loan granted to Women Youth & People with Disability Groups | 23 | - 186,459 | - |
| Loan recovered from Women, Youth & People with Disabilities | 23 | 62,132 | 221,810 |
| Acquisition of property, plant, and equipment & investment properties | 38 | - 935,975 | - 2,060,682 |
| **Net cash from investing activities** | | - 1,060,302 | - 1,838,873 |
| **Cash flows from financing activities** | | | |
| Interest on Loan | 27 | - 3,300 | - 3,055 |
| **Net cash used in financing activities** | | - 3,300 | - 3,055 |
| **Net increase in cash and cash equivalents** | | 1,192,450 | - 191,948 |
| Cash and cash equivalents at beginning of period | | 846,734 | 1,038,682 |
| Fund taken by MOF | 10 | - 7,981 | - |
| **Cash and cash equivalents at end of period** | 19 | 2,031,203 | 846,734 |

The financial statements were signed on behalf by:

Leah G. Kibaki
CMT Secretary
Date: 13/3/2021

Dionis M. Myinga
CMT Chairperson
Date: 13/3/2021

### 1.0 INDEPENDENT REPORT OF THE CONTROLLER AND AUDITOR GENERAL

**Hon. Chairperson of the Council,**
**Bukombe District Council,**
**P.O. Box 2,**
**BUKOMBE.**

### 1.1 REPORT ON THE AUDIT OF FINANCIAL STATEMENTS

**Qualified Opinion**

I have audited the financial statements of Bukombe District Council, which comprise the statement of financial position as at 30th June, 2020, and the statement of financial performance, statement of changes in net assets and cash flow statement and the statement of comparison of budget and actual amounts for the year then ended, as well as the notes to the financial statements, including a summary of significant accounting policies.

In my opinion, except for the effects of the matters described in the basis for qualified opinion section of my report, the accompanying financial statements present fairly in all material respects, the financial position of the Bukombe District Council as at 30th June, 2020, and its financial performance and cash flows for the year then ended in accordance with International Public Sector Accounting Standards (IPSAS) Accrual basis of accounting and in the manner required by the Local Government Finances Act 1982 (Revised 2019).

I conducted my audit in accordance with International Standards of Supreme Audit Institutions (ISSAIs). My responsibilities under those standards are further described in the Auditor's Responsibilities for the Audit of the financial statements section of my report. I am independent of Bukombe District Council in accordance with the International Ethics Standards Board for Accountants' Code of Ethics for Professional Accountants (IESBA Code) together with the National Board of Accountants and Auditors (NBAA) Code of Ethics, and I have fulfilled my other ethical responsibilities in accordance with these requirements.

I believe that the audit evidence I have obtained is sufficient and appropriate to provide a basis for my opinion.

### 1.2 REPORT ON COMPLIANCE WITH LEGISLATIONS

**Compliance with the Public Procurement Act,2011 (as amended in 2016)**

**Conclusion**

**Subject matter: Compliance audit on procurement of works, goods and services**

I performed compliance audit on procurement of works, goods and services in the Bukombe District Council for the financial year 2019/20 as per stipulations of Public Procurement Act, 2011 (as amended in 2016) and its regulation of 2013 (as amended in 2016).

**Conclusion**

Based on the audit work performed, I state that, procurement of goods, works and services of Bukombe District Councilis generally in compliance with the requirements of the Public Procurement Act No.7 of 2011 and its underlying Regulations of 2013 (as amended in 2016).

Charles E. Kichere
Controller and Auditor General
Dodoma, United Republic of Tanzania.
31st March, 2021

216445302

# NIT yaifagilia serikali kuanzisha usafiri SGR

Na Beatrice Moses

MKUU wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Prof. Zacharia Mganilwa, ameipongeza serikali katika mpango mkakati wa kuanzisha treni za umeme kwenye majiji makubwa, ambapo uchambuzi yakinifu umeshafanyika kwa Jiji la Dodoma ili kuanza mradi huo.

Alisema taifa lolote la uchumi wa kati lazima liwe na mahitaji ya treni za umeme, na kwamba ni habari njema kuona kuwa uchambuzi yakinifu umeshakamilika kwa Jiji la Dodoma kuwa jiji la kwanza nchini kuanzisha usafiri huo muhimu.

Prof. Mganilwa alimweleza Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara aliyefika chuoni hapo mwishoni mwa wiki kujionea utendaji kazi wa chuo hicho.

Alisema kufikia mwaka 2023/24 Taifa litakuwa na uzalishaji wa umeme wa kufikia megawati 5,000, hivyo kufanya mradi huo wa treni ya umeme kuwa wenye mafanikio makubwa.

Prof. Mganilwa alisisitiza kuwa chuo kinaendelea kuunga kuunga mkono miradi mikubwa ya serikali ikiwamo mradi wa reli ya kisasa (SGR), ujenzi wa meli, mafuta na gesi na vile vile katika eneo la uchumi wa bluu.

"Kwenye maeneo hayo yote tumeanzisha kozi mpya ambazo tutazalisha nguvu kazi ya kutosha kukidhi mahitaji."

Alimweleza Naibu Waziri kuwa katika kusaidia kuleta maendeleo katika eneo la uchumi wa bluu, chuo kimeanzisha shahada ya kwanza katika usanifu wa meli ili kusaidia mafanikio zaidi katika sehemu hiyo.

Kwa upande wake, Waitara aliisifia NIT kwa uwekezaji mkubwa wa miundombinu ya ufundishaji.

Waitara alisema kinafanya vizuri zaidi ya vyuo vyote ambavyo vipo kwenye Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi.

"Toka nimeanza kutembelea taasisi zilizo chini ya wizara yetu, chuo hiki ndiyo chuo bora kabisa. Wana vifaa vya kisasa vya kufundishia wanafunzi vyenye teknolojia bora, hivyo chuo hiki ni mfano wa kuigwa," alisema.

Alizitaka taasisi zilizo chini ya wizara hiyo kutenga muda na kutembelea NIT ili kujifunza jinsi ambavyo iliweza kupiga hatua kwenye mambo mbalimbali ya maendeleo ikiwamo uwekezaji katika miundombinu ya ufundishaji.

"Miradi ya kimkakati inaendelea chini ya Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan na tunatarajia kuona mradi wa reli ya umeme kuanza kwa majaribio mapema Novemba ambapo matarajio yetu ni kuajiri vijana wa kitanzania," alisema.

# Mrema awaomba viongozi wa dini vita dhidi ya corona

Na Thobias Mwanakatwe

MWENYEKITI wa Chama cha Tanzania Labour (TLP), Augustino Mrema, ameyataka madhehebu na viongozi wa dini nchini kuendelea kuwaelimisha waumini wao umuhimu wa kupata chanjo ya COVID-19 na kuchukua tahadhari za ugonjwa huo kama wataalamu wa afya wanavyoshauri.

Akizungumza juzi wakati wa misa takatifu ya shukrani kwa ajili ya kubariki nyumba yake na za watoto wake alizozijenga eneo la Salasala jijini Dar es Salaam, Mrema alisema janga la corona lipo, hivyo kila mtu ahakikishe anachukua tahadhari.

Misa hiyo iliendeshwa na Padri Folbertus Marandu wa Kanisa Katoliki Parokia ya Mtakatifu Augustine Salasala jijini Dar es Salaam.

"Napenda kulishukuru Kanisa Katoliki kwa kutoa elimu kwa waumini wao juu ya umuhimu wa chanjo ya corona ambayo ni hiari kwa anayetaka na shukrani za kipekee zimwendee Askofu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Mhashamu Yuda Ruwai'chi, ambaye amewahimiza mapdri kupata chanjo," alisema.

Mrema ambaye ni Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi mstaafu, alisema Watanzania waepuke propaganda zinazotolewa na baadhi ya watu wanaopinga chanjo ya corona wakati serikali imeileta ili kutusaidia kukabiliana na ugonjwa huo.

"Ruwai'chi sio kiongozi wa siasa, lakini anahimiza mapadri na waumini kuchanja chanjo ya corona, chanjo ni muhimu sana na ukinga watu wote wenye ugonjwa wa kisukari, presha, kifua kikuu pamoja na watu wenye umri wa miaka 60 kuchangamkia chanjo mapema kwani zinatolewa bure bila malipo," alisema.

Mrema alisema siyo mara ya kwanza kwa wananchi wa Tanzania kupata chanjo lakini inashangaza chanjo hii ya UVIKO-19 imekuwa na upinzani mkali sana na cha kushangaza miongoni mwa wanaopinga ni viongozi wa kisiasa.

" Kuchanja sawa na polisi anapokwambia funga mkanda unapokuwa kwenye gari, anakusaidia ili hata ukipata ajali huwezi kuumia sana sababu mkanda utakuzuia, " alisema.

Mrema alisema hofu ya kwamba waliochanjwa baada ya muda watakuwa mazombi hizo ni kauli za kuwatia hofu kwani wataalamu waliobobea na masuala ya afya duniani wameshathibitisha kuwa chanjo hiyo ni salama.

Alisema hakuna sababu ya kuingiwa na hofu katika suala hili kwani bahati nzuri hata Rais Samia Suluhu Hassan ameonyesha njia kwa kupata chanjo hiyo, ambayo inaendelea kutolewa katika nchi kadhaa duniani.

Naye Padri Marandu aliwataka waumini kujenga tabia ya kuvumiliana, kwani kunapokosekana uvumilivu tunajenga jamii ambayo haina baraka.

Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Agosti zaidi ya watu 300,000 wameshapata chanzo nchini.



Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara (katikati), akijionea ufanyaji kazi wa kituo cha ukaguzi wa magari kilichoko chini ya Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Soko usafiri wa kukodi lilivyopaa kwa kasi EA

Na Mwandishi Wetu

SEKTA ya usafirishaji imekuwa kwa haraka katika nchi nyingi barani Afrika kutokana na kuwapo kwa usafiri wa kukodi, ambapo wateja wanatafuta kupata usafiri salama na wenye gharama nafuu.

Ukanda wa Afrika Mashariki vilevile unashuhudia kukua kwa usafiri wa kukodi ambapo huduma mbalimbali kama Bolt wanatoa huduma kupitia katika mfumo wao uliyopo katika application ya simu.

Soko la kukodi usafiri kwa njia ya mtandao katika Afrika na Mashariki ya Kati lilitazamiwa kukua kufikia Dola bilioni 7.3 kufikia mwaka 2023. Sababu kubwa zinazochochea kuwapo kwa mahitaji ya usafiri wa kukodi katika kanda hii ni pamoja na kukua kwa miji, ongezeko la idadi ya vijana, kuongezeka kwa uwekezaji unaofanywa na watoa huduma za usafiri wa kukodi na ongezeko la idadi ya watumiaji wa simu za janja na mtandao wa internet.

Tanzania haiko tofauti na nchi nyingine, kutokana na ongezeko la watumiaji wa mtandao wa internet na simu janja, watu katika miji na majiji kama Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza na Arusha wanapata fursa ya kufurahia huduma ya usafiri wa kukodi ambayo imeleta mabadiliko makubwa katika namna ambavyo watu wa mijini wanavyosafiri.

Meneja wa Bolt Tanzania, Remmy Eseka, amesema huduma ya usafiri wa kukodi unashuhudia ukuaji mzuri.

"Mfumo wa usafiri wa kukodi kuendana na mahitaji ya Bolt unatoa njia rahisi na salama ya uombaji wa usafiri pale unapohitajika jambo ambalo linaloweza kuwezesha watumiaji kujipatia usafiri kama wanavyohitaji na kwa gharama nafuu," alisema Eseka na kuongeza

"Huduma zetu zinahakikisha kwamba wateja wanaweza kufahamu kwa usahihi ni wapi gari lilipo, wanaweza kufuatilia safari zao na wanaweza kuchukuliwa na kushushwa mahali popote wanapohitaji, jambo linalopelekea huduma zetu kuongezeka umaarufu.

"Bolt vile vile inachangia katika kukua kwa uchumi kwa madereva ambapo tunatoa mfumo wa Bolt kama chanzo kikuu na wakati mwingine kama chanzo cha ziada cha kiuchumi kwa madereva ambao wanataka kutekeleza majukumu mengine na wakati huo huo wakiwa wanaweza kuhudumia maisha yao," aliongeza.

Kwa mujibu wa Eseka, mfumo huu umewasaidia madereva kuwa na uwezo kamili wa kuutawala muda wao na kiwango cha fedha ambacho wanaweza kujipatia.

# Fursa ya soko la tumbaku yapatikana

BUNGE limeelezwa kuwa katika msimu wa kilimo wa mwaka 2020/21, Tanzania imepata masoko mapya ya kuuza tumbaku kwa majaribio katika nchi tatu.

Katika kutekeleza hilo, serikali inatarajia kukutana na uongozi wa kampuni ya TLTC mwishoni mwa mwezi Septemba, 2021 ili kuirejesha.

Wizara ya Kilimo ilitoa majibu hayo bungeni jana ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Uramb,o (CCM), Margaret Sitta.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kuwezesha kampuni za wazawa ili yawalipe wakulima mara wanaponunua Tumbaku yao.

"Suala la kupata wanunuzi zaidi wa kununua Tumbaku ni la muda mrefu; Je kuna mafanikio yaliyopatikana?" alihoji.

Katika majibu ya Wizara hiyo, ilisema serikali inaendelea na jitihada za kutafuta soko la tumbaku katika nchi mbalimbali hasa nchi za Uarabuni, Afrika na Ulaya.

Ilitaja masoko hayo mapya ya majaribio kuwa ni katika nchi ya Romania (tani 200), Poland (tani 100) na Uturuki (tani 50).

Aidha, ilisema sampuli za tumbaku zimetumwa nchini China na Korea Kusini kwa ajili ya masoko hayo.

Kwa mujibu wa Wizara hiyo, kwa muda mrefu biashara ya tumbaku imekuwa ikiendeshwa bila kampuni za kizawa kushiriki katika biashara ya Tumbaku na kampuni za nje pekee ndizo zilikuwa zinashiriki katika biashara ya tumbaku.

Ilisema wakati wa ununuzi wa tumbaku kupitia kampuni za nje ununuzi wa tumbaku umeshuka hadi kufikia tani 42,000 za mkataba na baada ya kampuni za wazawa kuingia katika ununuzi uzalishaji umeongeza kufikia tani 68,571 za tumbaku kupitia kilimo cha mkataba.

Aidha, katika masoko ya tumbaku msimu wa kilimo 2020/21 jumla ya kampuni tisa zinanunua tumbaku ya wakulima zikiwemo kampuni saba za wazawa.

Hata hivyo, ilisema kampuni hizo zimekuwa zikikabiliwa na kero ya kupata mitaji ya kutosha hali inayosabisha kuchelewa kuwalipa baadhi ya wakulima.

"Katika kutatua changamoto hiyo, Mei, 2021 Wizara ya Kilimo ilikutanisha kampuni za wazawa na taasisi za fedha kwa lengo la kukubaliana masharti nafuu yatakayowezesha kampuni hizo kupata mikopo kwa riba nafuu," ilisema.

Ilieleza kuwa mafanikio ya majadiliano hayo yameanza kupatikana ambapo benki ya CRDB imeridhia kuzikopesha kampuni mbili za Mo Green International na Magefa Growers Limited.

Ilisema serikali inaendelea kushirikiana na kampuni za ununuzi wa tumbaku na taasisi za fedha katika kutatua kero hiyo kwa lengo la upatikanaji wa soko la uhakika la tumbaku na malipo ya wakulima kwa wakati.

Wizara ilisema ni muhimu kama nchi kuendelea kulea makampuni ya wazawa ili yawe na uwezo wa kununua tumbaku kama makampuni ya kigeni na kuyaunganisha makampuni ya wazawa taasisi za kifedha ili kupata huduma za kifedha ikiwemo kupata Letter of Credit (L.C).



Mbunge wa Jimbo la Urambo, Magreth Sitta, akiwa ameinama kwenye ya kiti Bungeni Dodoma jana, baada ya kukatisha swali lake kwa kudai kuwa anauchungu kutokana na wakulima wa tumbaku jimboni kwake kutolipwa fedha za madai ya mauzo ya zao hilo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Walioathiriwa miradi mkakati kufidiwa mwaka huu wa fedha

IMEELEZWA kuwa wakazi wa Jiji la Dodoma ambao viwanja vyao vimeathirika na miradi ya kimkakati watalipwa fidia mwaka wa fedha 2021/22.

Miradi hiyo imetajwa kuwa ni wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) na njia ya umeme wa msongo wa 400kv kutoka Chalinze -Zuzu.

Wananchi hao ni wale ambao walishafanyiwa uthamini na baadhi yao wamekwishalipwa fidia na wengine wanaendelea kuhakikiwa na watalipwa kwa mwaka huo.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), ilitoa kauli hiyo bungeni jana ilipokuwa ikitoa majibu katika swali la Mbunge wa Viti Maalum, Conchesta Rwamlaza.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji lini serikali itawalipa fidia wananchi wenye viwanja eneo la Miganga West na East Kata ya Mkonze katika Jiji la Dodoma kwa kuwa uthamini ulishafanywa na baadhi yao bado kulipwa.

Katika majibu ya Ofisi hiyo, ilisema eneo la Miganga West na East liko katika Kata ya Mkonze ni miongoni mwa maeneo ya Halmashauri ya Jiji la Dodoma ambayo yamepangwa, kupimwa viwanja na kumilikishwa wananchi ili waviendeleze kwa mujibu wa Mpango Kabambe wa Mji Mkuu (Master Plan).

Ilisema kufuatia uwepo wa miradi ya kimkakati wa ujenzi wa SGR na ujenzi wa njia ya umeme inayotekelezwa na serikali kupita katika eneo hilo na kuathiri viwanja vilivyomilikishwa imelazimu eneo hilo kutwaliwa chini ya Sheria ya Utwaaji Ardhi namba 47 ya 1967, Sheria ya Ardhi Na. 4 ya 1999, Kanuni za Ardhi za 2001, Miongozo ya Uthamini na Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini Na. 7 ya 2016.

## Maelfu ya vijana wapewa ushauri wa fursa za ajira

SERIKALI imesema katika kipindi cha Julai 2016 hadi Juni 2021, mawakala wa ajira nchini wamechangia vijana 39,273 kupata huduma ya ushauri.

Ofisi ya Waziri Mkuu ilibainisha hayo bungeni jana ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Pangawe (CCM), Haji Amour Haji.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema kwa vile serikali imeruhusu uwapo wa Mawakala wa Ajira nchini, ina mkakati gani juu ya ajira za nje.

"Je, ni upi mchango wa Mawakala wa ajira hapa nchini?" alihoji.

Katika majibu ya Ofisi hiyo ilisema pia vijana 19,509 wamepewa mafunzo ya watafutakazi, vijana 11,371 wameunganishwa na fursa za mafunzo ya utarajali na vijana 10,554 wameunganishwa na fursa za kazi ndani na nje ya nchi.

Awali, ilibainisha kuwa serikali imeweka mikakati mbalimbali ya kuwasadia vijana kupata ajira za nje ya nchi ikiwa ni pamoja na kubaini nchi za kimkakati zenye fursa za ajira za staha na kuingia makubaliano na nchi husika.

Ilisema makubaliano hayo ni kuwajengea uwezo vijana wa kitanzania kuwa na ujuzi utakaowawezesha kushindania fursa za ajira nje ya nchi.

Pia, kujenga mfumo wa huduma za ajira ambao pamoja na mambo mengine utarahisisha utafutaji wa kazi nje ya nchi, kuweka mwongozo wa kuratibu shughuli za Wakala Binafsi wa huduma za ajira wanaopeleka watu nje ya nchi na kufanyia marekebisho Sheria ya Huduma za Ajira ya mwaka 1999 pamoja na kanuni zake za Mwaka 2014 ili kuendana na mazingira ya sasa.




Habari zote na Augusta Njoji



Ukurasa 14

**Kufunza uwekezaji, ujasiriamali wanaostaafu ni sawa lakini...**



Ukurasa 12

Misango; mbunifu asiyesomea ufundi aunda trekta aina yake



Ukurasa 13

Mimba za wanafunzi zilivyomliza mzazi

ELIMU

## NA SABATO KASIKA

# Kurejeshwa waliokatisha masomo wizara inapotajiwa kasoro, utatuzi

SERIKALI imetangaza mpango wa kuwarejesha shuleni mabinti waliokatisha masomo kwa sababu mbalimbali ikiwamo mimba, utekelezaji wake ukitarajiwa kuanza rasmi mwakani.

Wasichana hao watasoma katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs) takribani 41, vilivyoko nchi nzima vilivyoandaliwa, kwa ajili ya kuwapokea.

Baadhi ya wadau wakiwamo walimu wanautizama mkakati huo na kuchambua kasoro na kutoa mapendekezo kwa serikali, ili kuufanya uwe wa kiufanisi zaidi.

Suzan Lyimo ni mwalimu mstaafu wa Sekondari ya Jangwani, jijini Dar es Salaam, anayetofautiana na mpango huo, kwa maelezo kwamba unafanana na ule Mpango wa Elimu kwa Waliokosa (MEMKWA), uliolenga kundi hilo wakati wa awamu ya tatu.

"Njia nzuri ambayo ingesaidia ni kuruhusu waliopata mimba kurudi katika shule zao, kama kawaida au wahamishiwe shule za jirani, waendelee na masomo kuliko kutengewa madarasa katika vyuo," anasema Suzan.

Susan ambaye alikuwa mbunge wa CHADEMA kwa miaka kadhaa na Waziri Kivuli wa Elimu, anasema, haamini kwamba wanafunzi waliopata mimba na kujifungua, wakirudi shuleni wanaweza kuwa mfano mbaya kwa wengine na kwamba dhana hiyo, haina msingi.

"Ukweli ni kwamba kuna haja ya kujiandaa kikamilifu, kwa sababu hata silabasi yake haijulikani na hatujui hao wanafunzi watafundishwa na nani, sidhani kama watapata elimu ya kawaida, inakuwa ni MEMKWA," anasema.

Mwalimu huyo mstaafu anaeleza kuwa siasa zingeachwa kwenye suala hilo, ili kusaidia watoto wa kike waliokatisha masomo kuendelea na shule, hatimaye watimize ndoto zao walizojiwekea kwenye elimu.

### KASORO ZINGEREKEBISHWA

Katibu Mkuu wa Chama cha Kutetea Haki na Maslahi ya Walimu Tanzania (CHAKAMWATA), Meshack Kapange, anasema huo mpango ni mzuri, lakini unahitaji kufanyiwa kazi zaidi.

"Binafsi siamini kama vyuo hivyo 54 vinaweza kutosha, pia suala la walimu na gharama za bweni kwa ajili ya wanafunzi hao atalipa nani? Pengine serikali inatakiwa kulifanyia kazi zaidi suala hili."

Anafafanua kuwa wapo wanafunzi waliokuwa wanasoma shule za vijijini ambako hakuna vyuo hivyo, walikuwa wanaenda shule na kurudi nyumbani na kwamba kuwapeleka katika vyuo hivyo ni kunaongeza gharama.

"Si hapo tu, hao wanafunzi watafundishwa na walimu gani? Ni hao wa vyuo au watatoka sekondari? Ikumbukwe kuwa shule nyingi nchini zina uhaba wa walimu. Yaani kwa ujumla ninaona huu mpango unatakiwa kufanyiwa kazi zaidi," anasema.

Kapange anasema, njia bora ambayo serikali ingetumia kuwasaidia wanafunzi hao ni kuruhusu wasomee katika shule za maeneo walioko kabla, badala ya kuwapeleka mbali hali, ambayo inaweza kuongeza gharama kwa wazazi.



Meshack Kapange, Katibu Mkuu wa CHAKAMWATA. **PICHA: MTANDAO**

### MPANGO NI MZURI ILA...

Rais mstaafu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Gratian Mkoba, anasema, mpango huo ni mzuri, lakini anahisi kwamba unaweza kuchangia kushamiri kwa mimba nchini iwapo hakutakuwa na mikakati ya kuimarisha.

"Ni kwamba, kuna faida na hasara kwenye mpango huu, lakini njia pekee ni kuimarisha maadili na uchumi, ili kuondokana na mimba hizi, ambazo zimekuwa zikikatisha ndoto za watoto wetu," anasema Mkoba.

Mkoba anasema, mimba zinachangiwa na mambo mawili ambayo ni umaskini kwenye jamii, pia ukosefu wa maadili, ambapo anashauri mambo hayo yaimarishwe, ili kuwa na jamii ambayo haitakubali vitendo hivyo.

"Bila kuhimiza hayo, ili jamii iwe kwenye mstari, baadhi ya wanafunzi wanaweza kuona kuwa suala la mimba kama jambo la kawaida, kwani vyuo vipo, wakiamini kwamba hata wakipata mimba na kupelekwa huko," anasema.

Mwalimu huyo anataka jamii isielemewe na dhambi na badala yake iishi vizuri na kwamba vinginevyo tatizo hilo linaweza kuendelea kuwapo na kusababisha hata mpango wa serikali kukwama.

"Tuimarishe maadili na uchumi katika jamii, ndiyo njia nzuri ambayo inaweza kusaidia kupunguza tatizo, pia mpango huo kuwa na matokeo bora, kwani wapo wanafunzi wanapata mimba katika mazingira ya kubakwa," anasema.

INAENDELEA UK.12

TEKNOLOJIA

**NA ANTHONY GERVAS, MWANZA**

# Misango; mbunifu asiyesomea ufundi aunda trekta aina yake

LIVINUS Misango mkazi wa Mji wa Kisesa, wilayani Magu mkoani Mwanza, amechoka na jembe la mkono na kuamua kuunda trekta analoliita la kienyeji, linalotokana na kuunganisha vyuma kwa kutumia utundu na utaalamu wake binafsi.

Katika simulizi yake anasema ametumia teknolojia ya kienyeji ya kukusanya vyuma vilivyotumika na kuunda kitendea kazi hicho alichokifanikisha kutokana na utundu, ili kuchochea kipaji chake kwa lengo la kujiajiri.

Misango anaeleza; “Nataka kuondoa changamoto katika kilimo na kurahisisha ulimaji, awali sikuwa na vitendea kazi kwenye kilimo mbali na jembe la mkono, lakini sasa nimeunda trekta, kwa sasa ndiyo tegemeo langu kulima mazao ya chakula na biashara.”



Trekta la Misango likiwa kazini kwa kubeba abiria. **PICHA: ANTHONY GERVAS**

### UFUNDI BILA SHULE

Misango licha ya kuunda trekta hilo, anasema fani yake ni mtaalamu wa kompyuta, lakini hajawahi kusomea ufundi katika chuo chochote kiwe cha ufundi au cha VETA bali ni utundu wake, dhamira na kipaji ndivyo vitu vilivyofanikisha kupata mafanikio hayo.

Amefikia uamuzi wa kujiajiri mwenyewe baada ya kumaliza kidato cha sita na kuona nafasi za ajira ni chache na kuwashauri vijana waache kusubiria ajira, kwani zipo kazi nyingi za kujiajiri wao wenyewe, zinazoweza kuwakomboa kiuchumi na kimaisha.

Anasema trekta hilo linaunganishwa na majembe ya plau (yale yanayokokotwa na ng'ombe ) na kulima ekari tano, kwa siku na likifungwa trela hubeba watu sita wakati wa kwenda shambani.

> “Alipoanza kutengeneza trekta watu waliojaribu kumkatisha tamaa kuwa hataweza kuunda kitendea kazi hicho...

“Injini niliyoifunga ikifungwa mota inaweza kutumika kuvuta maji kumwagilia mazao shambani, ilikuwa ni vigumu kwenda dukani kununua trekta kutokona na hali ya uchumi. Ubunifu na utundu wangu umekuwa ni silaha tosha ya kujikwamua kimaendeleo na kiuchumi,” anaeleza.

Anasimulia kuwa ameunda trekta hilo, ili kurahisisha na kufanikisha kilimo cha mahindi, mpunga, pamba na maharage pamoja na viazi na mazao mengine ya kibiashara.

Anasema tangu kuunda trekta amefanikisha kujenga nyumba yenye thamani ya Shilingi milioni 6.1 na kusisitiza kuwa kipaji chake kitampeleka mbele zaidi hata kuunda vitu vingine vyenye tija au manufaa kwake na kwa jamii akisema la lazima na umhimu ni mtu kuwa na uthubutu.

### MANUFAA YA TREKTA

Misango anabainisha kwamba kazi za trekta aliloliunda ni pamoja na kulima eka tano kwa siku, kuvuta maji kwa ajili ya umwagiliaji shambani, kupukuchua mahindi, kupiga mpunga na kuvuna, pia ikifungwa mota inafua umeme.

“Haliishii hapo linakokota trela na kubeba mazao mbalimbali, bidhaa, nafaka magunia zaidi ya 15 ya mahindi au mpunga, vile vile husomba mbolea na kupukuchua mahindi magunia 50 kwa siku na kubeba zaidi ya tani moja.” Anasema.

Anajigamba kwamba pamoja na kuweka pembeni kwa muda shughuli za ufundi na kujikita kwenye kilimo shambani, anaamini ujuzi hauzeeki.

“Ujuzi hauzeeki,mtu ndiye anazeeka,kazi ya ufundi nimeiweka pembeni kwanza, ili nifanye shughuli za kilimo ambacho nimegundua pia kina tija ukizingatia kanuni za kilimo bora shambani, nikichoka na kilimo bado nina nafasi ya kujiendeleza na ufundi, anasema Misango.

### USHAURI KWA VIJANA

Anawashauri vijana kufanya kazi kwa kujituma wasibweteke, kujikita kwenye kujifunza mambo mbalimbali kama kujaribu ubunifu, teknolojia na kujitambua kuwa ni lazima kujituma.

Anawataka kuwa na uthubutu, tena uchukue nafasi ya muhimu, ili waweze kujiajiri wenyewe badala ya kutegemea ajira serikalini au kwenye sekta binafsi, ambazo ni adimu wakati huu.

Lakini, anasema kitu kingine muhimu anachoamini katika maisha yake ni kukataa mawazo potofu ya watu mbalimbali unapokuwa umeazimia kufanya jambo lenye tija. Hilo linaweza kukukwamisha na kutamani kuliacha au kuachana na mpango wako, ambao ungekuwa na umuhimu.

Anasema alipoanza kutengeneza trekta hilo wapo watu waliojaribu kumkatisha tamaa kuwa hataweza kuunda kitendea kazi hicho, lakini aliwapuuza.

Anakumbusha kwamba kote duniani ajira hazitoshi, lakini kuna nafasi kubwa ya kujiajiri na kutumia teknolojia ya kuanzisha hata kiwanda chochote cha kutengeneza bidhaa au malighafi za aina mbalimbali zikiwamo za kilimo.

## Kurejeshwa waliokatisha masomo wizara inapotajiwa kasoro, utatuzi

**INATOKA UK.11**

Rais huyo anasema, anaamini wapo wenye ndoto na vipaji ambavyo wanatamani vitumike, lakini wakapata mimba, hivyo wakipewa nafasi wanaweza kuitumia vizuri.

“Pamoja na hayo nisisitize kuwa, kwenye mpango kuna matokeo mawili, ambayo ni faida na hasara. Yaani kuna wanafunzi wanaoweza kufanya vizuri zaidi, pia wengine wanapoona wenzao waliopata mimba wanarudishwa kuendelea na masomo, wanaweza kushawishika kupata mimba,” anasema.

### MIPANGO YA SERIKALI

Hivi karibuni serikali ilitangaza kuanza kuwarejesha masomoni mabinti waliokatisha masomo, kwa sababu mbalimbali ikiwamo mimba wakiwa shuleni, ambao utaanza ramsi mwaka 2022.

Chini ya utaratibu wa kuboresha elimu ya sekondari Tanzania (SEQUIP), mabinti hao sasa watapata nafasi ya kuendelea na masomo yao waliyokatisha katika mfumo wa elimu wa kawaida.

Mpango huo unatumia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs) kusomesha mabinti hao, ambapo kwa sasa inaelezwa kuwa utaanza kutekelezwa kwenye vyuo 41 kati ya 54, vilivyopo nchini.

Katika juhudi za kufanikisah mpango huo, serikali imeshaagiza vyuo vyote vya FDCs vilivyoko chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuanza kuwadahili mabinti hao kuanzia mwakani.

Wakuu wa vyuo hivyo 41 wameshaelekezwa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk Leonard Akwilapo kusajili vyuo vyao kuwa vituo vya kufanyia mitihani ya kidato cha nne na kidato cha pili, ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wa kike waliokumbwa na matatizo hayo, wanarudi na kuendelea na masomo.

ELIMU

**NA JULIETH MKIRERI, KISARAWE**

# Mimba za wanafunzi zilivyomliza mzazi



Wanafunzi wakisoma katika mazingira magumu. **PICHA: MTANDAO**

MAISHA yangu yalianza kubadilika mwaka 2011, baada ya kutengana na mume wangu Abdallah Juma, na kuniachia jukumu la kulea familia.

"Haikuwa kazi rahisi. Maisha yangu yalitegemea ukulima hasa vibarua, ili kumudu mahitaji kama chakula, elimu na afya kwa watoto tena mabinti watatu, wakisoma shule za msingi na sekondari."

Ndivyo anavyosema mama mzazi Mwanahawa Chakupewa, mkazi wa Kijiji cha Makurunge, mkoani Pwani, katika ushuhuda wake, kuwa licha ya kujitahidi usiku na mchana kuwatunza mabinti, walitumbukia kwenye mtego wa ujauzito.

Anaeleza kuwa maisha ya kuhangaikia vibarua kwake yalikuwa magumu, lakini hana budi kuendelea nayo, ili watoto wapate chakula kila siku.

Mwanahawa anasema kuwa elimu kwa mabinti hususani wanaotoka kwenye familia maskini inakwamishwa na mambo mengi, lakini suala la kukosa fedha ni changamoto inayosababisha kutumbukia kwenye mimba za utotoni.

Watoto hunarubuniwa na watu wanaowaahidi kuwapa mahitaji, ambayo hawayapati kwa wazazi au walezi wao na kusababisha kupata mimba udogoni na shuleni pia, anaongeza.

Anasema wanaowahadaa hutumia umaskini wa wazazi na walezi na kuwaingiza kwenye tamaa ya kupata huduma mbalimbali na mwisho kuangukia kwenye mimba za utotoni.

**KILICHOMKATISHA TAMAA**

Anasimulia mkasa wa mabinti zake wawili kukatisha masomo kutokana mimba anazoamini zimechangiwa na umaskini wa familia kwa kushindwa kuwapatia fedha za kujikimu.

"Maisha yalianza kubadilika mwaka 2011, nilitelekezwa na mume aliyeniachia watoto haikuwa rahisi nikipata pesa kutoka kwenye kazi za vibarua," anasimulia mzazi huyo.

Aidha, mtihani mkubwa ulikuwa ni kupata Sh. 500 kila siku za kuwapa watoto wakienda asubuhi, jambo analolita pasua kichwa, anasema.

"Watoto wangu siku wakienda shule na Sh. 500, kwa kila mmoja ujue ni mara moja kwa mwezi na hiyo ni baada ya kununua unga na maharage inayobakia nawapa. Lakini muda mwingi walikuwa wakienda bila chochote," anaeleza.

Anakumbusha: "Kuna wakati walinilalamikia kuwa wanahitaji fedha ya kununua vitu shuleni, lakini sikuwa na majibu mbali na uchungu."

**MIMBA ZIMEWAKWAMISHA**

Kutokana na hali hiyo Mwanahawa anaeleza kuwa ni chanzo cha kukatisha masomo baada ya kupata mimba kwa kukubali kupewa fedha, ili wafanane na wengine wenye pesa za kujikimu.

Mwanahawa anasema: "Anayeniumiza zaidi ni yule aliyekatisha masomo akiwa darasa la tano katika Shule ya Msingi Makurunge, ambaye hadi leo haijulikani anaishi wapi na nani, kwa sababu alitoroka."

"Nilikwenda kuripoti polisi, lakini sikufanikiwa kumpata wala kumjua aliyempatia ujauzito mwanangu," anasema kwa majonzi na kueleza kuwa amekata tamaa, licha ya kusema anampigia simu mara kwa mara akimtaka atulie kwani yuko salama.

"Nilimtafuta bila mafanikio baadaye alikuwa akinipigia simu na kuniambia kutokana na hali ya hapa nyumbani bora aondoke akatafute maisha yake, ili asizidi kunisononesha," anasimulia Mwanahawa.

Wakati akiendelea kutafakari maisha mapya mbali na binti huyo ambaye ameondoka nyumbani akiwa mdogo na ujauzito, machungu yake yaliendelea kwani binti yake mwingine aliyekuwa kidato cha kwanza amekatisha masomo baada ya ujauzito.

Anasema alikuwa anasoma Sekondari ya Makurunge naye hasomi na amebaki nyumbani baada ya kupata mimba.

Mwanahawa anasema alijiona amebeba mzigo mzito kwani pamoja na kujituma kuwahangaikia ili wasome, walimlipa machozi kwa kukatisha masomo kwa mimba.

Anasema kabla ya binti yake huyo kuanza kidato cha kwanza, aliongea naye kirafiki mara kwa mara akitaka kujua kama kweli anataka kusoma, ili amnunuliwe mahitaji.

"Nilimhoji mara kwa mara, ili nisiingie hasara kutokana na maisha yangu kuwa magumu, lakini alinihakikishia anataka masomo na hatahangaika," anasimulia mzazi huyo .

Mwanahawa anasema hata mwaka haukumalizika binti yake alianza kulalamika anaumwa hawezi kwenda shule..."Ilianza siku hadi mwezi kila siku ikiwa na kisingizio cha kutokwenda shule," anaeleza.

"Wiki zilivyokatika nililazimika kwenda shule kutoa taarifa kwa walimu kuhusiana na kuumwa kwa mwanangu, lakini nilivyoona sababu zinazidi nilitumia namna ya tofauti ya maongezi tuliyoyazoea ndipo aliposema hawezi tena kwenda shule ana mimba," anaeleza.

> Hadi sasa sijajua wale vijana waliohusika kumpatia mwanangu mimba wako wapi na hapa mtaani hawajaonekana tena.

Anasema alitoa taarifa shuleni kwa mara nyingine pia alifika polisi, lakini binti yake hakutoa ushirikiano kumtaja mwanamume aliyempa ujauzito.

Mwanahawa anasema mabinti zake huenda kuna vitu vikubwa walivihitaji, ambavyo waliamini mama yao hana uwezo navyo, hivyo wakajiingiza kwenye uhusiano uliowapa mimba wangali wanafunzi.

Mmoja wa wahitimu wa Sekondari Makurunge, Tatu Juma binti wa Mwanahawa anasema, kilichowafanya ndugu zake kupata ujauzito ni kudanganywa na kuingizwa kwenye tamaa.

Anaeleza kuwa yeye pamoja na wadogo zake walikuwa wakienda shule bila kula chochote hadi jioni wanaporejea nyumbani, lakini alivumilia kwakuwa alikuwa na malengo na alikataa kushawishiwa.

Anasema mdogo wake aliyepata ujauzito akiwa kidato cha kwanza alimpa wakati mgumu shuleni, huku kila mmoja akimtabiria kuwa hata yeye atapata ujauzito kutokana na hali duni ya nyumbani kwao.

Anasema "Nilifanikiwa kuruka vikwazo vingi hadi nilipohitimu na sasa nasubiri kuendelea na masomo ya kidato cha tano natamani kumkomboa mama yangu."

Ibrahimu Hamad, mkazi wa Kiluvya ambaye mtoto wake alikatisha masomo kwa kupata ujauzito akiwa darasa la tano, anaeleza kuwa mabinti wanadanganywa.

Hamad anamlalamikia mtoto wake kurubuniwa na mfanyakazi wa ng'ombe aliyemuahidi kumpa fedha, hivyo kutoroka nyumbani kwao na kuhamia kwa kijana huyo licha ya baba yake kumpatia kila alichokihitaji.

Anasema baada ya kumkosa binti yake nyumbani kwa siku tatu alilazimika kutoa taarifa polisi na vijana wawili walikamatwa kwa tuhuma za kumuweka kinyumba na baadaye aligundulika ni mjamzito hivyo kukatisha masomo.

Anasema alikwama kufuatilia kesi polisi kutokana na kukosa fedha na ushirikiano mdogo wa polisi.

"Hadi sasa sijajua wale vijana waliohusika kumpatia mwanangu mimba wako wapi na hapa mtaani hawajaonekana tena," anasema.

Anasema ameshindwa kuendelea kufuatilia kesi ya binti yake kutokana na kukosa nauli ya mara kwa mara kwenda polisi, badala ya kutumia fedha kumhudumia mwanae na mjukuu wake.

ELIMU

NA REUBENI
LUMBAGALA, DODOMA

# Kufunza uwekezaji, ujasiriamali wanaostaafu jambo jema, lakini...




Wafanyakazi wafunzwe ujasiriamali wakiwa na nguvu si wakati wanapokaribia kustaafu. **PICHA: MTANDAO**

MFANYAKAZI anapoajiriwa katika utumishi wa umma au sekta binafsi upo wakati atastaafu na kuachana na ajira kwa mujibu wa sheria au kwa hiari.

Mwajiriwa huyo anaweza kustaafu kwa hiari anapofikisha umri wa miaka 55 au kwa lazima anapotimiza miaka 60, sheria za kazi zinaelekeza.

Pia kwa mujibu wa sheria hizo, wafanyakazi hupaswa kuchangia fedha kutoka katika mishahara yao kati ya asilimia tano hadi 10, ili kujiwekea akiba katika mifuko ya hifadhi ya jamii ya PSSSF au NSSF.

Waajiri nao hupaswa kuwachangia wafanyakazi wao kati ya asilimia 10 hadi 15 ya ngazi za mishahara ya watumishi wao, ili kutunisha mafao ya wafanyakazi wao.

Muda wa kustaafu, aidha kwa hiari au kwa lazima unapofika, mfanyakazi anastaafu huku mifuko ya hifadhi ya jamii ya PSSSF na NSSF ikitoa mafao kwa mtumishi kwa kadri alivyochangia pamoja na ile michango ya mwajiri wake.

Hapo ndipo mfanyakazi anapoingia katika mfumo mpya wa maisha ya kustaafu utumishi wake akiwa amepata mafao yake.

> “Waajiri nao hupaswa kuwachangia wafanyakazi wao kati ya asilimia 10 hadi 15 ya ngazi za mishahara ya watumishi wao, ili kutunisha mafao ya wafanyakazi wao.

Serikali, vyama vya wafanyakazi na taasisi za fedha zimekuwa zikiandaa mafunzo ya ujasiriamali kwa wafanyakazi wanaotarajia kustaafu miezi michache kabla ya kufikia hatua hiyo.

Pamoja na mafunzo hayo kuwa yenye tija katika kuwaelekeza wastaafu watarajiwa juu ya matumizi bora ya mafao yao hasa kiuwekezaji, lakini ukweli ni kuwa mafunzo hayo yanatolewa kwa kuchelewa mno.

Kumfundisha mstaafu mtarajiwa masomo ya uwekezaji na fursa za kiuchumi miezi michache kabla ya kuondoka kwenye ajira ni jambo jema, lakini mafunzo hayo ya ujasiriamali na uwekezaji yanapaswa kutanguliwa na mafunzo kadhaa aliyopata mfanyakazi huyo miaka ya nyuma kabla hata ya kuwaza lini atastaafu utumishi wake. Kinachotakiwa apate wakati huo ni mafunzo ya kuboresha uwekezaji aliotakiwa kuwa amefunzwa miaka kadhaa kabla.

Naamini, wafanyakazi wakipewa mafunzo ya ujasiriamali na ya kiuwekezaji muda mchache baada ya kuajiriwa, itawasaidia kuzitambua fursa mbalimbali, ambazo wakiwekeza mitaji yao wataweza kuinuka kiuchumi wangali vijana tena wakiwa kazini.

Kutokana na ukweli kuwa mishahara haitoshi na wala haitokuja kutosheleza mahitaji ya wafanyakazi hasa kutokana na gharama za maisha kuwa juu kugharamia kodi ya nyumba, umeme, maji, chakula, matibabu, usafiri, kusomesha watoto na mahitaji mengine, ni muhimu kwa wafanyakazi kuwa na vyanzo mbadala vya kuwaingizia kipato achilia mbali mishahara wanayoipata kutoka kwa waajiri wao.

Kutokana na hali hii, waajiri wanapaswa kuwatengenezea wafanyakazi wao mazingira bora ya kukabiliana na maisha kwa kuwaandalia semina za ujasiriamali na uwekezaji na kuwafuatia, ili waweze kuinuka kiuchumi na hatimaye kufanyakazi kwa ufanisi bila kuwa na msongo wa mawazo wa hali ngumu za maisha zinazowakabili.

Wafanyakazi wana fursa ya kupata mikopo kutokana na kuaminika katika taasisi za fedha kama vile benki na vikundi vya kukopa na kukopesha SACCOS.

Huu ni mwanzo mzuri kwa wafanyakazi kuwa na mitaji ya kuwekeza katika biashara, kilimo, ufugaji na washauri elekezi (consultants). Hivyo basi, wafanyakazi wawekewe mazingira bora ya kupata mafunzo ya ujasiriamali, biashara na uwekezaji, ili watakapokopa mikopo waweze kuwekeza sehemu sahihi kutokana na fursa za mafunzo walizopata mapema.

Utaratibu wa sasa wa mafunzo kutolewa hasa unapofika wakati wa kustaafu huenda usiwe na tija kwa wastaafu kwani katika umri wao wa uzee wanapata wakati mgumu kusimamia biashara na uwekezaji wanaoanzisha hali inayosababisha baadhi yao kupata msongo wa mawazo na hata wengine kupoteza maisha pale uwekezaji wake unaposhindwa kutoa matokeo waliyoyatarajia. Endapo mafunzo yakitolewa mapema muda mfupi au miaka michache baada ya kuajiriwa, wafanyakazi watawekeza sehemu sahihi na hata kukitokea changamoto ya mitaji yao kutotoa matokeo mazuri, watakuwa na nafasi nyingine ya kurekebisha pale walipokosea awali.

Waajiri wanaweza kuandaa semina na mafunzo ya ujasiriamali wao wenyewe au kuomba wataalamu kutoka kwa taasisi au mashirika mengine, ili kutoa mafunzo hayo, ili kuwajengea uwezo wafanyakazi katika fursa mbalimbali za ujasiriamali, ili kuwainua kiuchumi.

Vilevile, vyama vya wafanyakazi wanao wajibu wa kurudisha sehemu ya michango inayochangwa na wanachama wao kugharamia mafunzo ya ujasiriamali kutoka kwa wataalamu wa biashara, uwekezaji na uchumi.

Taasisi za fedha kwa upande wao katika kuongeza wigo wa wateja na kutanua huduma za fedha wagharamie mafunzo ya ujasiriamali kwa wafanyakazi, ili waweze kukopa katika taasisi zao, ili kuwasaidia kuinuka kiuchumi huku mabenki nayo yakipata faida kupitia mikopo waliyoitoa. Wafanyakazi wakiwekeza mapema wangali vijana, hawatatetereka utakapofika muda wa kustaafu kwani watakuwa na uelewa na uzoefu wa kutosha katika biashara.

Pia, hata mafao watakayopata watayatumia katika kupanua biashara na uwekezaji wao na si kuanzisha biashara au uwekezaji mpya, ambao unawaletea wakati mgumu katika usimamizi na ufuatiliaji kutokana na umri wao kuwa mkubwa, pia kukosa uzoefu wa kutosha.

***Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali, iliyoko Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.***
***Maoni: 0620-800462.***





# Wanaoingiza dawa za kulevya kukiona

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, amesema serikali imejipanga kuendelea kuwachukulia hatua za kisheria watu wanaojihusisha na uingizaji wa dawa za kulevya.

Mhagama, alibainisha hayo juzi alipokuwa akizungumza na wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Masuala ya Ukimwi pamoja na asasi za kiraia zinazoshirikiana na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA).

Alisema Mamlaka hiyo chini ya Kamishna Jenerali Gerald Kusaya, kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi inaendelea kuhakikisha kuwa vitendo hivyo vinadhibitiwa.

Mhagama alisema dawa hizo zimekuwa zikileta madhara makubwa kwa Watanzania kiafya na kusababisha huduma za tiba kwa Watanzania kuwa kubwa ikiwamo kuporomoka kwa uchumi.

Waziri Mhagama, aliongeza kuwa matumizi ya dawa za kulevya yanasababisha magonjwa sugu kama ukimwi, homa ya ini, TB na mengineyo na kupotea nguvu kazi ya Taifa kwani asilimia 56, ya nguvu kazi ya Taifa ni vijana ambao ni watumiaji wa dawa hizo kwa wingi.

"Kwa mara ya kwanza tangu tupate uhuru muda mfupi baada ya uteuzi wa Kamishna Jenerali, Gerald Kusaya, Tume ilikamata dawa za kulevya mchanganyiko kilo 859.36 kwa mara moja huku ikidhibitiwa mipenyo iliyokuwa ikitumika kuingiza mingine tofauti na ile ambayo iliyokuwa imezoeleka kama ya Dar es Salaam, Bagamoyo na Tanga."

Maeneo mengine alisema ni mikoa ya kusini, Lindi na Mtwara kwenye fukwe za bahari, ambapo kama siyo umahiri na upambanaji wa mamlaka wasingeweza kufikia hatua hiyo.

Hata hivyo, alisema bado kuna tatizo la unyanyapaa kwa wanaotumia au waliowahi kutumia dawa za kulevya na wakaacha.

Alisema suala hilo limekuwa tatizo linalotakiwa kufanyiwa kazi kuona ni jinsi gani hali hiyo inamalizika ili kuwaruhusu wengine kujitokeza wapate tiba na warudi wakawe raia wema.

Naye Naibu Waziri anayeshughulikia Kazi, Vijana na Ajira, Patrobas Katambi, alibainisha kuwa janga hilo linaleta shida katika nyanja ya diplomasia, afya na maendeleo ya vijana ambo ndiyo nguvu kazi ya taifa.

"Tunaahidi kufanya utafiti pamoja na kwamba kazi zinafanyijka katika mamlaka za mikoa, lakini naona kuna haja ya kuongeza nguvu tujue chimbuko, athari na viashiria vya uwapo wa dawa za kulevya na twende tukaangalie namna ya kuongeza rasilimali fedha za kuwasaidia waraibu wa dawa za kulevya," alisema Katambi.

# Mfumo wa stakabadhi ghalani sasa kuboreshwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeahidi kufanya maboresho ya kero zinazojitokeza kwenye mfumo wa stakabadhi ghalani ikiwamo kufanya mapitio kwenye sheria na kanuni ili uwe na tija kwa wakulima nchini.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, aliyasema hayo katika semina iliyotolewa na wizara hiyo kwa wabunge kutoka kamati tano za Bunge kuhusu utekelezaji wa mfumo huo.

Kamati hizo ni ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, Kamati ya Bajeti pamoja na Kamati ya Hesabu za Serikali.

Akizungumza kwenye semina hiyo, Kigahe alisema mfumo huo unasaidia kuweka bei shindani yenye tija kwa wakulima.

"Serikali ina mikakati ya kutatua changamoto ambazo zimejitokeza katika kutekeleza mfumo huu ikiwa ni pamoja na kuboresha kujenga maghala mengi ili kupunguza changamoto za wakulima wadogo kupeleka maghala ya umbali hivyo tuendelee kujenga maghala mengi ili kuhifadhi mazao yetu na kupata bei nzuri," alisema.

Alisema pia serikali inaendelea kusajili maghala na kukaribisha wadau kujenga kwa kuwa ni biashara nzuri ili kusaidia kuhifadhi mazao na kuuza kwa bei nzuri.

Hata hivyo, alisema wameweka wakaguzi ili kudhibiti ujanja ujanja unaofanywa wa kuwapunja wakulima.

"Pia kukagua ubora kabla ya kuhifadhi ghalani kama Mbunge Kunti alivyoshauri kukagua ubora ili kuhakikisha bidhaa unayolipwa iwe halali na haijachanganywa na vitu," alisema.

Kadhalika, alitoa wito kwa wabunge wa Kanda ya Ziwa kuanza kutoa elimu kwa wananchi kulima kilimo biashara kwa kuwa mazao ya choroko na dengu yana soko na kuahidi serikali itatoa elimu kwa kanda hiyo.

Awali, Kaimu Mkurugenzi Mkuu Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB), Asangye Bangu, alisema dhumuni la kuanzishwa mfumo huo ni kukuza juhudi za serikali kurasimisha mifumo ya masoko iliyopo ili kupunguza vipingamizi mbalimbali vinavyokwaza uzalishaji wenye tija.

Bangu amesema mfumo huu una manufaa mbalimbali ikiwamo kuwapa nguvu wawe kamili hususani wakulima kupigania bei nzuri katika soko kwa kuhamasisha kutumia mfumo wa pamoja kukusanya na kuuza, kutoa uhakika wa ubora na bidhaa na Mfumo wa uthibitisho, kupunguza mashaka na gharama za ushughulikiaji kwa wafanyabiashara wa bidhaa na wakulima wakati wa kufanya biashara.

Alisema mfumo huo umesaidia kuweka utaratibu wa kupata taarifa na takwimu za soko na mauzo za kuaminika kwa wadau mbalimbali, kuongeza ushiriki wa wafanyabiashara wa bidhaa wenyeji katika biashara ya kimataifa, kuhimiza usindikaji nchini wa mazao ya msingi kwa lengo la kuongeza thamani nakukuza uendelezaji wa viwanda.

Naye Mrajisi Mkuu wa Tume ya Vyama vya Ushirika nchini, Dk. Benson Ndiege, alisema mfumo huo ukiimarishwa utakuwa mkombozi wa mkulima na kwamba Tume hiyo imeshaanza mchakato wa kukusanya maoni na kurekebisha Sheria ya Ushirika.



Rais wa Chama cha Madaktari wa Kikristo Tanzania (TCMA), Dk. Bwire Chirangi, akizungumza wakati wa ufunguzi wa mkutano mkuu wa 84 wa mwaka wa madaktari hao uliofanyika jana jijini Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wahandisi wakumbushwa kujisajili ERB

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIBU Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga, amewataka wahandisi ambao hawajajisajili kwenye Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB) kutimiza matakwa ya sheria.

Sanga, alitoa rai hiyo juzi wakati wa kufunga mkutano wa 18, wa Siku ya Wahandisi Tanzania uliofanyika jijini Dodoma kwa siku mbili.

Alisema ni vyema wahandisi kujisajili kwa sababu ni takwa la kisheria na hakuna njia nyingine ya kufanya ili watambulike na bodi hiyo.

Aidha, aliwataka kuchangamkia fursa ya kujiunga na mpango wa mafunzo kwa wahitimu unaosimamiwa na ERB, ili kusajiliwa ndani ya muda mfupi wa miaka mitatu.

"Wahandisi ni lazima kujisajili kwenye bodi kwani ni takwa la kisheria ili utambulike unatakiwa kujisajili na siyo vinginevyo," alisisitiza Sanga.

Pia, Sanga aliwasihi waajiri katika sekta ya kihandisi au kampuni za kihandisi kuona namna ya kuwachukua wahitimu wa uhandisi ili kuwapatia fursa ya kupata uzoefu jambo ambalo litawasaidia kusajiliwa na kuajiriwa haraka.

Awali, Msajili wa ERB, Patrick Barozi, alisema mpaka sasa bodi hiyo imesajili wahandisi 31,729 na kati ya hao wanawake ni 3,344 sawa na asilimia 12.

Aidha, Balozi aliwataka wahandisi 632 waliokula kiapo kuishi kwenye kiapo hicho kwa uaminifu na kutambua kuwa Taifa limeweka matumaini makubwa kwao na mategemeo ya kiwango cha juu cha weledi kwenye majukumu yao ya kila siku.

Kadhalika, alitoa wito kwa waajiri nchini ambao wanaajiri wahandisi kuwa na mipango mahusisi ya kuwaruhusu na kuwagharamia ili kila mwaka washiriki katika mikutano hiyo muhimu ya kitaaluma.



# Jela kwa kukutwa na karatasi za kutapeli

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MTU mmoja mkazi wa Ilomba, jijini Mbeya amehukumiwa kifungo cha miaka saba jela baada ya kupatikana na kosa la kukutwa na karatasi za kutapelia watu.

Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mbeya, imemhukumu kwenda jela mshtakiwa Masoud Salim (32), baada ya kuthibitika kuwa mshtakiwa amewatapeli watu mbalimbali katika jamii na kuwaachia huru mshtakiwa wa pili, Amos Mahenge na mshtakiwa wa tatu James Antony, baada ya ushahidi wa mashahidi watatu wa upande wa mashtaka kutowagusa. Akirejea ushahidi wa baadhi ya mashahidi hao wa Jamhuri, Hakimu Mkazi Mfawidhi Mkoa wa Mbeya, Zawadi Laizer, alisema serikali imethibitisha kwamba mshtakiwa huyo wa kwanza alikuwa na tabia ya utapeli baada ya kukamatwa na vyombo vya dola Machi 26, 2020 nyumbani kwake Sae.

Baada ya kupekuliwa alikutwa na vitu vyenye kemikali kwa ajili ya kuwadanganya watu, chupa zenye kemikali na karatasi kadhaa mfano wa noti za Sh. 10,000 kwa ajili ya kutengeneza noti bandia kitendo ambacho kilielezwa na upande wa mashtaka kuwa ni kinyume na kifungu namba 341 A cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 ya mwaka 2019.

Hakimu Laizer alisema mshtakiwa alikana kutenda kosa hilo licha ya awali kukiri na kuwataja mshtakiwa wa pili na watatu kuwa ndiyo amekuwa akishirikiana nao huku akikumbusha kwamba mshtakiwa aliyehukumiwa aliwahi kukimbia kwa zaidi ya miezi mitatu wakati wa mwenendo wa kesi hiyo na kusitisha kwa muda usikilizwaji wa kesi hiyo hadi alipokamatwa baadaye huko Rujewa Mbarali.

Baada ya kutiwa hatiani Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Wakili Davice Msanga, aliiomba mahakama kutoa adhabu stahiki kama sheria inavyoelekeza ili iwe fundisho kwa jamii kutokana na kushamiri kwa vitendo vya utapeli ikiwamo kutumia dawa huku mshtakiwa Masoud akiiomba mahakama kumpunguzia adhabu kwa kuwa ni kijana anayetegemewa na familia hasa mke na watoto.

Baada ya maelezo ya pande zote mbili Hakimu Mkazi Mfawidhi Mkoa wa Mbeya, Zawadi Laizer, alimhukumu mshtakiwa Masoud Salim kwenda kutumikia adhabu ya kifungo cha miaka saba jela na kuwaachia huru mshtakiwa wa pili na wa tatu baada ya kutokutwa na kesi ya kujibu huku akiweka wazi haki ya kukata rufani kwa upande usioridhika na uamuzi wa mahakama yake.




Mkurugenzi wa Shirika la Elimisha mkoani Mbeya, Festo Sikagonamo, akizungumza na watumishi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, (hawapo pichani) juu ya umuhimu wa upangaji bajeti kuanzia ngazi ya familia juzi kwenye ukumbi wa shirika hilo. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# GIZ kuandaa mpango usalama wa maji

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WADAU wa maji mkoani Mbeya, serikali na Shirika la Maendeleo la Watu wa Ujerumani (GIZ), wameanza kuandaa mpango wa usalama wa maji utakaowezesha Mamlaka ya Majisafi na Salama mkoani hapa kutoa huduma bora na endelevu kwa wananchi.

Wadau wa maji mkoani haa wakiongozwa na maofisa kutoka Wizara ya Maji wamekutana kwa lengo la kuandaa mpango wa usalama wa maji ambao utawahakikishia wananchi huduma ya uhakika ya upatikanaji wa majisafi na salama.

Mkemia Mwandamizi kutoka Wizara ya Maji, Stanley David, yupo mkoani hapa kuandaa mpango wa usalama wa maji (Water Safe Plan) kwa lengo la kuhakikisha jitihada za serikali kuwapatia wananchi huduma hiyo zinafanikiwa kwa kiasi kikubwa.

"Wizara inaendelea na kukagua na kuhakikisha usalama wa maji unaanzia kwenye chanzo cha maji hadi kwa watumiaji na kutatua matatizo yanayowakabili," alisema David.

Akizungumzia mpango huo, mwakilishi wa Shirika la GIZ, Samwel Sudi, alisema shirika hilo kwa kushirikiana na Wizara ya Maji wanatekeleza mradi kusaidia Mamlaka za Maji, Mbeya, Songwe na Tunduma kuandaa mpango wa usalama wa maji kwa kuhakikisha zina uwezo wa kuzalisha maji yenye bora na ya kutosha.

Ofisa Uhusiano wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (UWSSA), John Nkana, alisema mpango huo utasaidia upatikanaji wa maji kwa Jiji la Mbeya na viunga vyake.

Alisema mradi huo utajikita kuangalia usalama wa maji kuanzia chanzo, usambazaji na kutibu kwa watumiaji ili kupunguza matatizo yanayotokana na majisafi na salama.

# Mbegu bora madume ya ng'ombe yazaa matunda

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

UPATIKANAJI wa mbegu bora za madume ya ng'ombe kwa wafugaji wilayani Rungwe, mkoani Mbeya umechochea ongezeko kwa uzalishaji wa zao la maziwa kwa kuzalisha lita 200,000 kwa siku na kuingizwa sokoni.

Mwenyekiti wa Muungano wa Chama cha Wafugaji wilayani Rungwe (MUHAMARU), Asha Lukaja, alisema hayo kwenye elimu ya kutumia teknolojia za kisasa za ufugaji kwa kuwatumia maofisa ugani waliosambazwa wilayani humo na Kampuni ya Asasi kwa kushirikiana na Serikali ya Denmack nchini Tanzania kwa lengo la kuwawezesha wafugaji kuzalisha maziwa kwa tija na kuingiza katika mnyororo wa thamani.

Alisema kabla ya elimu hiyo walikuwa wakikabiliwa na tatizo la masoko na mbegu bora, Kiwanda cha Maziwa cha Asasi kimewapatia madume ya mbegu bora za ng'ombe ambayo yamesaidia ongezeko la majike na kuchochea ongezeko la uzalishaji wa zao la maziwa.

"Licha ya ongezeko la uzalishaji wa maziwa na uwepo wa masoko ya uhakika bado tatizo kwa baadhi ya wafugaji kuingiza sokoni maziwa yasiyokuwa na ubora jambo linalochangia kuchafua na kutia doa maziwa yanayozalishwa wilayani Rungwe," alisema Lukaja.

Miongoni mwa wafugaji wilayani Rungwe, Fadhili Mbilinyi, alisema kuwapo kwa kampuni za ununuzi wa maziwa wilayani Rungwe kumeleta tija wa wafugaji kuongeza uzalishaji na kufuga kisasa.

Alisema kwa sasa wanazalisha kiasi kikubwa cha maziwa na uhakika wa upatikanaji wa soko ndani na nje ya wilaya hiyo.

Ofisa Mifugo Wilaya ya Rungwe, Dk. Dennis Kamily, alisema wafugaji wengi hawapendi kuwatumia maofisa ugani kujifunza namna bora ya kuzalisha maziwa bila kutumia vyakula visivyo salama kwa ng'ombe.

Mkaguzi wa Maziwa Wilaya ya Rungwe, Henry Mokiwa, alisema asilimia 20 ya maziwa yanayozalishwa na wafugaji wilayani humo yanakosa ubora kutokana na baadhi ya wafugaji kuongeza maji.

"Ukamuaji wa maziwa kiholela kwa baadhi ya wafugaji kunachangia kuzalisha bakteria 500 hadi 1,000 kila baada ya saa tatu na kusababisha madhara kwa watumiaji na kushauri wafugaji kuwatumia maofisa ugani ili kuboresha sekta ya maziwa nchini," alisema Mokiwa.

# Fursa ya soko la tumbaku yapatikana

BUNGE limeelezwa kuwa katika msimu wa kilimo wa mwaka 2020/21, Tanzania imepata masoko mapya ya kuuza tumbaku kwa majaribio katika nchi tatu.

Katika kutekeleza hilo, serikali inatarajia kukutana na uongozi wa kampuni ya TLTC mwishoni mwa mwezi Septemba, 2021 ili kuirejesha.

Wizara ya Kilimo ilitoa majibu hayo bungeni jana ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Uramb,o (CCM), Margaret Sitta.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kuwezesha kampuni za wazawa ili yawalipe wakulima mara wanaponunua Tumbaku yao.

"Suala la kupata wanunuzi zaidi wa kununua Tumbaku ni la muda mrefu; Je kuna mafanikio yaliyopatikana?" alihoji.

Katika majibu ya Wizara hiyo, ilisema serikali inaendelea na jitihada za kutafuta soko la tumbaku katika nchi mbalimbali hasa nchi za Uarabuni, Afrika na Ulaya.

Ilitaja masoko hayo mapya ya majaribio kuwa ni katika nchi ya Romania (tani 200), Poland (tani 100) na Uturuki (tani 50).

Aidha, ilisema sampuli za tumbaku zimetumwa nchini China na Korea Kusini kwa ajili ya masoko hayo.

Kwa mujibu wa Wizara hiyo, kwa muda mrefu biashara ya tumbaku imekuwa ikiendeshwa bila kampuni za kizawa kushiriki katika biashara ya Tumbaku na kampuni za nje pekee ndizo zilikuwa zinashiriki katika biashara ya tumbaku.

Ilisema wakati wa ununuzi wa tumbaku kupitia kampuni za nje ununuzi wa tumbaku umeshuka hadi kufikia tani 42,000 za mkataba na baada ya kampuni za wazawa kuingia katika ununuzi uzalishaji umeongeza kufikia tani 68,571 za tumbaku kupitia kilimo cha mkataba.

Aidha, katika masoko ya tumbaku msimu wa kilimo 2020/21 jumla ya kampuni tisa zinanunua tumbaku ya wakulima zikiwemo kampuni saba za wazawa.

Hata hivyo, ilisema kampuni hizo zimekuwa zikikabiliwa na kero ya kupata mitaji ya kutosha hali inayosababisha kuchelewa kuwalipa baadhi ya wakulima.

"Katika kutatua changamoto hiyo, Mei, 2021 Wizara ya Kilimo ilikutanisha kampuni za wazawa na taasisi za fedha kwa lengo la kukubaliana masharti nafuu yatakayowezesha kampuni hizo kupata mikopo kwa riba nafuu," ilisema.

Ilieleza kuwa mafanikio ya majadiliano hayo yameanza kupatikana ambapo benki ya CRDB imeridhia kuzikopesha kampuni mbili za Mo Green International na Magefa Growers Limited.

Ilisema serikali inaendelea kushirikiana na kampuni za ununuzi wa tumbaku na taasisi za fedha katika kutatua kero hiyo kwa lengo la upatikanaji wa soko la uhakika la tumbaku na malipo ya wakulima kwa wakati.

Wizara ilisema ni muhimu kama nchi kuendelea kulea makampuni ya wazawa ili yawe na uwezo wa kununua tumbaku kama makampuni ya kigeni na kuyaunganisha makampuni ya wazawa taasisi za kifedha ili kupata huduma za kifedha ikiwemo kupata Letter of Credit (L.C).



Mbunge wa Jimbo la Urambo, Magreth Sitta, akiwa ameinama kwenye ya kiti Bungeni Dodoma jana, baada ya kukatisha swali lake kwa kudai kuwa anauchungu kutokana na wakulima wa tumbaku jimboni kwake kutolipwa fedha za madai ya mauzo ya zao hilo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Walioathiriwa miradi mkakati kufidiwa mwaka huu wa fedha

IMEELEZWA kuwa wakazi wa Jiji la Dodoma ambao viwanja vyao vimeathirika na miradi ya kimkakati watalipwa fidia mwaka wa fedha 2021/22.

Miradi hiyo imetajwa kuwa ni wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) na njia ya umeme wa msongo wa 400kv kutoka Chalinze -Zuzu.

Wananchi hao ni wale ambao walishafanyiwa uthamini na baadhi yao wamekwishalipwa fidia na wengine wanaendelea kuhakikiwa na watalipwa kwa mwaka huo.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), ilitoa kauli hiyo bungeni jana ilipokuwa ikitoa majibu katika swali la Mbunge wa Viti Maalum, Conchesta Rwamlaza.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji lini serikali itawalipa fidia wananchi wenye viwanja eneo la Miganga West na East Kata ya Mkonze katika Jiji la Dodoma kwa kuwa uthamini ulishafanywa na baadhi yao bado kulipwa.

Katika majibu ya Ofisi hiyo, ilisema eneo la Miganga West na East liko katika Kata ya Mkonze ni miongoni mwa maeneo ya Halmashauri ya Jiji la Dodoma ambayo yamepangwa, kupimwa viwanja na kumilikishwa wananchi ili waviendeleze kwa mujibu wa Mpango Kabambe wa Mji Mkuu (Master Plan).

Ilisema kufuatia uwepo wa miradi ya kimkakati wa ujenzi wa SGR na ujenzi wa njia ya umeme inayotekelezwa na serikali kupita katika eneo hilo na kuathiri viwanja vilivyomilikishwa imelazimu eneo hilo kutwaliwa chini ya Sheria ya Utwaaji Ardhi namba 47 ya 1967, Sheria ya Ardhi Na. 4 ya 1999, Kanuni za Ardhi za 2001, Miongozo ya Uthamini na Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini Na. 7 ya 2016.

## Maelfu ya vijana wapewa ushauri wa fursa za ajira

SERIKALI imesema katika kipindi cha Julai 2016 hadi Juni 2021, mawakala wa ajira nchini wamechangia vijana 39,273 kupata huduma ya ushauri.

Ofisi ya Waziri Mkuu ilibainisha hayo bungeni jana ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Pangawe (CCM), Haji Amour Haji.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema kwa vile serikali imeruhusu uwapo wa Mawakala wa Ajira nchini, ina mkakati gani juu ya ajira za nje.

"Je, ni upi mchango wa Mawakala wa ajira hapa nchini?" alihoji.

Katika majibu ya Ofisi hiyo ilisema pia vijana 19,509 wamepewa mafunzo ya watafutakazi, vijana 11,371 wameunganishwa na fursa za mafunzo ya utarajali na vijana 10,554 wameunganishwa na fursa za kazi ndani na nje ya nchi.

Awali, ilibainisha kuwa serikali imeweka mikakati mbalimbali ya kuwasadia vijana kupata ajira za nje ya nchi ikiwa ni pamoja na kubaini nchi za kimkakati zenye fursa za ajira za staha na kuingia makubaliano na nchi husika.

Ilisema makubaliano hayo ni kuwajengea uwezo vijana wa kitanzania kuwa na ujuzi utakaowawezesha kushindania fursa za ajira nje ya nchi.

Pia, kujenga mfumo wa huduma za ajira ambao pamoja na mambo mengine utarahisisha utafutaji wa kazi nje ya nchi, kuweka mwongozo wa kuratibu shughuli za Wakala Binafsi wa huduma za ajira wanaopeleka watu nje ya nchi na kufanyia marekebisho Sheria ya Huduma za Ajira ya mwaka 1999 pamoja na kanuni zake za Mwaka 2014 ili kuendana na mazingira ya sasa.



# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## PATA MKOPO

PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA ENTEPRISES FINANCE LIMITED (EFL). KWA MAWASILIANO ZAIDI

**TUPIGIE:0677 111 333**

**AU 0758 112 332**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

## KUPOTEA KWA CHETI



**CHARLES J MAGOMA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1072-0061** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary KAMENE mwaka 2015, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **WMB/RB/327/2021**

116442602

## KUPOTELEWA NA CHETI



**Amisa Juma Paul mkazi wa Mwasele** Manispaa ya Shinyanga. Anatangazo kupotelewa na Cheti cha Kidato cha Nne chenye Index namba **S4208-0003** na **CS15 01011684,** kilichotolewa na baraza la mitihani Tanzania kupitia shule ya Sekondari Eloni iliyopo Babati mwaka 2015. Yeyote atakae kiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Amisa Juma Paul kwa simu namba **0768220752. RB/SHY/RB/2021/ Control namba 9910830152089.**

116443302

## KUPOTEA KWA CHETI



**LAURYN DEUS OWDEN** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.0265-0013 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **CORNELIUS** mwaka **2018** ,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochotecha polisi Polisi taarifa
**DAR/KIL/ RB/431635/2021**

## TANGAZO KUPOTEA OFA YA KIWANJA

**Juma Jumanne** mkazi wa Ndala Manispaa ya **Shinyanga.** Anatangaza kupotelewa na Ofa ya kiwanja **Namba 109/4 Kitalu "HH" (HD)** kilichopo maeneo ya Ndala Manispaa ya Shinyanga. Kwa yeyoye atakaekiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Juma Jumanne kwa simu namba **0742450920** Rbnamba/ **SHY/RB/2021/Control namba 9910823669390.**

116442902

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MOHAMED ENTEPRISES (T) LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **BOXER** yenye namba za **MC 300 CNU,** chasis namba **MD2B15BYOLWM88478,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **DAR/CEN/RB/426624/2021**

216443002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya DODOMA.**

**Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA.**

**Usimamizi wa mirathi Na 36/2021.**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU KEYA RAMADHANI SALUMU WA DODOMA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA MAULIDI O. MASANGU**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na Mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 07 mwezi 09 mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
**Zingatia;** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 25 mwezi 08 mwaka 2021.

116442802

**RE: THE LAND ACT NO 4 OF 1999**

**LOSS OF ORIGINAL LETTER OF OFFER**
**LOSS OF ORIGINAL LETTER OF OFFER OF;**
**REF; NO. MMC/LD/11477**

**REGISTERED OWNER: HEMEDI JUMA**

**LAND 328 BLOCK ``B" LOCATION TUNGI**

**APPLICANT:ASIA MOHAMED ATHUMANI**

**TAKE NOTICE** that the **ORIGINAL LETTER OF OFFER to** the land described above is said to be lost and that I intend to issue a **REPLACEMENT OF THE ORIGINAL OF OFFER** in lieu thereof unless cause to the contrary is shown within thirty days from the date of this publication.

The **ORIGINAL LETTER OF OFFER** is found should be delivered to the office of the Municipal Director, Morogoro Municipality council,P.O.BOX 166 Morogoro

Tumaini D. Mayugwa
For; MUNICIPAL DIRECTOR,
MOROGORO

116443202

TWINS AUCTION MART CO.LTD & COURT BROKER
P.O.Box1305 Songea,

30/08/2021

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

KWA IDHINI TULIYOPEWA NA MAHAKAMA YA MWANZO MFARANYAKI SONGEA MJINI. TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA NYUMBA YA MDAIWA ALLY ALFRED MLALILA NYUMBA KIWANJA NA 234, KITARU "JJ" ILIYOPO ENEO LA MITAWA WILAYA YA SONGEA KESI YA MADAI NA.4/2021 KATI YA FULGENSI SIMON KYANDO DHIDI YA ALLY ALFRED MLALILA. MNADA UTAFANYIKA TAREHE 24/9/2021 SIKU YA IJUMAA KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA.

**MASHARTI YA MNADA.**
MNUNUZI WA NYUMBA ATAKAYE BAHATIKA ATATAKIWA KULIPA 25% YA BEI ILIYOFIKIWA PAPO HAPO NA KIASI KILICHOBAKI KILIPWE NDANI YA SIKU 14, KINYUME CHA HAPO PESA ILIYOTOLEWA AWALI HAITARUDISHWA NA MNADA UTARUDIWA TENA. GHARAMA ZA KUBADILISHA HATI MILIKI (TRANSFER OF OWNER SHIP) NA GHARAMA NYINGINE HASA USAFIRI NI ZA MTEJA MWENYEWE NA NYUMBA ITAANZA KUKAGULIWA KUANZIA TAREHE YA TANGAZO HILI.

**Kwa mawasiliano zaidi wasiliana na:-**
**MKURUGENZI**
**TWINS AUCTION MART CO.LTD**
**S.L.P 1305,**
**SONGEA**
**SIMU NA. 0754881926, 0716070298,0784718734**

WOTE MNAKARIBISHWA

116442702

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJ

**ABEID HAMISI MOHAMED** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA BAJAJ YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 629 BYW. CHASSIS NAMBA MD6M14-PA4J4D11893. ENGINE NAMBA AK4DJ4515266.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **MDL/RB/2424/2021.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AHMED HUSSEIN OMARY** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **MITSUBISHI CANTER** yenye namba za usajili **T 253 BQM** , yeyote atakayeiokota atoe taarifa klituo chochote cha polisi Polii taarifa **ARU/MON/RB/473848/2020**

116443802

K-FINANCE

**MAJEMBE AUCTION MART LTD (VIJANA WA KAZI**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

KWA NIABA YA K-FINANCE LTD TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA WA MAGARI YA WADAIWA WALIOTAJWA HAPO CHINI.

MAHALI: YADI YA MAJEMBE MWANANYAMALA

| JINA LA MDAIWA | DHAMANA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|
| SHEDRACK ELINAMI MSHANGA | GARI AINA YA COLORA SPACIO NUMBER T 448 DJU | JUMAMOSI 13/09/2021 SAA 5:00 ASUBUHI |
| HAMIS ANTONY KINOTAH | GARI AINA YA VOLKSWAGEN TOURAGE NUMBER T 407 CQM | JUMAMOSI 13/09/2021 SAA 5:00 ASUBUHI |

**MASHARTI YA MNADA**

1. MNUNUZI ATALIPA HELA YOTE ILIYOFIKIWA KWENYE MNADA
2. GHARAMA ZA KUBADILISHA UMILIKI NI ZA MNUNUZI
3. KWA MAELEZO ZAIDI

**WASILIANA NASI KWA SIMU NAMBA 0715 980025, 0764 525253, 0714 465105**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**PONGWE WILAYA YA TANGA**
**Usimamizi wa Mirathi No. 30/2021**

Ombi la **HAMIDA ABDI MWAITA** Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu **MWANABORI MOHAMED HAJI**
Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo **tarehe 13/09/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
**Tarehe 20/08/2021.**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Wiki 1 tani 100,000 mahindi zinunuliwe

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimetoa wiki moja kwa serikali kununua tani 100,000 za mahindi kutokana na baadhi ya wakulima wa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kukosa masoko.

Aidha, kimezitaka Wizara ya Kilimo na Wizara ya Fedha na Mipango, kujadiliana kuhusu kupunguza gharama ya mbolea kwa wananchi.

Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Alisema wakulima wamehamasika, wamelima kwa bidii na wajibu wa serikali ni kuhakikisha kunakuwa na soko la uhakika la mazao yao.

Chongolo aliongeza kuwa serikali ilitenga Sh. bilioni 14, kwa ajili ya kununua mahindi kwenye mikoa mbalimbali ya wakulima, lakini taarifa alizonazo fedha kwa sasa zimeisha.

"Taarifa tulizonazo kutoka kwa viongozi wa chama kwenye mikoa ambayo Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA), inanunua mahindi tumeambiwa fedha zimekwisha na sasa zoezi la kununua linasuasua, tukasema hatuwezi kukaa namna hii, wakulima wetu wana mahindi hawana sehemu ya kuuza.

"Maagizo yetu kwa serikali watafute fedha wanapojua na zoezi la kununua mahindi liendelee kwenye maeneo yote, ambayo tulikubaliana mahindi yaendelee kununua, hadi sasa tunaambiwa wamenunua wastani wa tani 25,000 -28,000 na sisi CCM tunaagiza wanunue tani 100,000," alisema.

Pia, alisema taarifa ya Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) inaonesha kuwa mwaka huu kutakuwa na tatizo la mvua hazitanyesha kwa kiwango chenye tija na hivyo kutishia mwaka ujao kuwapo na uhaba wa chakula.

Akizungumzia kuhusu uchache wa vituo vya kununulia mahindi, alitaka NFRA watakapoanza kutekeleza agizo la kununua tani hizo za mahindi kusogeza vituo vya kununulia, ili kuwaondolea adha ya usafiri wakulima.

"Kuna malalamiko hii Sh. 500 kwa kilo wamekuwa wakikatwa sehemu ya fedha kwa madai kuwa ni ya usafiri, hii ni kumuonea mtu anayeishi mbali na mjini, CCM inasema mtu aliyepo eneo lolote mahindi yanunuliwe kwa bei hiyo, ili kuwa na bei sawia kwa wakulima wote na suala la usafiri lisiwe mzigo kwa wakulima," alisema.

Alisema Sekretarieti ya CCM itakwenda kwenye mikoa hiyo baada ya wiki moja kuangalia utekelezaji wa maagizo iliyotoa kwa kununua mazao bila masharti.

Kuhusu mbolea, alisema bei imepanda kwa kiwango kikubwa nchini na CCM iliahidi kuwalinda wakulima, licha ya tatizo hilo kuwa la dunia na kuagiza serikali kupitia wizara zake wakae waanze kujadiliana namna ya kupunguza mzigo wa gharama kwa wananchi.

## NEMC yaitoza faini Lake Oil ya bil. 3.3/-

**Na Joseph Mwendapole**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limeitoza faini ya Sh. bilioni 3.3, Kampuni ya Mafuta ya Lake Oil inayotuhumiwa kujenga vituo vingi vya mafuta maeneo mbalimbali, bila kuwa na vyeti vya Tathmini ya Athari za Mazingira (EIA).

NEMC imemtaka mmiliki wa kampuni hiyo kulipa faini hiyo ndani ya siku 14, kuanzia leo na asipofanya hivyo itatumia sheria kuvifungia vituo vyake vyote 66, nchini.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, wakati akizungumza na waandishi wa habari, ambapo alisema wamefikia hatua hiyo baada ya malalamiko ya wananchi wengi katika maeneo, ambayo vituo hivyo vinajengwa.

Alisema NEMC imebaini ongezeko kubwa la ujenzi wa vituo vya mafuta, ambavyo katika uchunguzi wao wamebaini kuwa vingi havina vibali vya ujenzi wala vyeti vya EIA.

Dk. Gwamaka alitoa siku saba kuanzia leo kwa vituo vyote, ambavyo vimejengwa bila kuwa na vibali vya EIA kufika kwenye ofisi za NEMC, kwa ajili ya kutoa maelezo kwanini visichukuliwe hatua.

Alisema imepita miaka 17 tangu sheria ipite na NEMC imetoa elimu kupitia njia mbalimbali, lakini wenye vituo vingi wameonyesha ukaidi hivyo muda wa kuchukua hatua kali umefika. Alisema hakuna asiyeona vituo vya mafuta vinaibuka katika kasi, ambayo ni ya ajabu sasa kwa muda NEMC imekuwa ikijiuliza mbona haioni vituo hivyo kwenda kujisajili kupata EIA.

Alisema kuwa kanuni zinataka umbali wa kituo kimoja cha mafuta hadi kingine usipungue mita 200, ili kuepusha athari kubwa zinazoweza kutokea wakati dharula ya moto, lakini kutokana na dharau ya wenye vituo hawazingatii kanuni hiyo.



Timu ya wahandisi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wakipata mafunzo kutoka kwa Kampuni ya New Forests, kampuni endelevu ya mbao, inayofanya kazi katika kiwanda cha kutibu miti mkoani Iringa. Lengo la mafunzo hayo ni kuwapa ujuzi, kuhakikisha ubora wa kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa mradi wa 2 wa umeme vijijini (REA) III awamu ya pili. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Atuhumiwa kuua mume kwa dawa za mganga aache pombe

**Na Halima Ikunji,** TABORA

JESHI la Polisi mkoani Tabora linamshikilia mwanamke aitwaye Mbaru Mwagembe, kwa tuhuma za kusababisha kifo cha mumewe.

Anadaiwa kumnywesha dawa aliyopewa na mganga wa kienyeji ya kumwezesha mumewe kuacha pombe.

Taarifa iliyotolewa na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora, Safia Jongo, ilieleza kuwa mwanaume huyo amefahamika kwa jina la Talibona Nyerere (47), kwamba alinyweshwa dawa hiyo inayodhaniwa kuwa ni sumu na mke wake mdogo.

Kamanda Jongo alisema tukio hilo lilitokea Septemba 3, mwaka huu katika Kitongoji cha Mtakuja, Kijiji cha Mwanzwilo, Kata ya Igusule, wilayani Nzega mkoani Tabora.

Alisema kwamba mwanamke huyo alimpa mume wake dawa hiyo wakati amerejea kutoka kunywa pombe ili kumsaidia aache kutumia kinywaji hicho.

Kamanda Jongo alisema ilikuwa ni kawaida ya mwanamke huyo kumpa dawa hiyo mume wake kila aliporejea kutoka kunywa pombe, kwamba alikuwa akifanya hivyo kutokana na maelekezo aliyopewa na mganga wa kienyeji.

Kamanda Jongo alisema baada ya kuhojiwa, mwanamke huyo alimtaja mganga huyo na kwamba kwa sasa anashikiliwa na jeshi hilo.

MECHI KALI
HOME
AWAY
TANZANIA
2.35 | 2.85 | 3.14
MADAGASCAR

1
WEKA PESA.
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4 - WEKA PESA.
vodacom m-pesa airtel money tigo pesa EZYPESA
- FUNGUA MENYU YA HALOPESA
- CHAGUA LIPA/LIPIA BILI
- WEKA NAMBA YA KAMPUNI 150888, KUMBUKUMBU 888.
- KISHA WEKA 500 AU ZAIDI.
SEND
halopesa

2
WEKA BET.
- PIGA *150*87#
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE KASINO

# CHELSEA YAJITOSA KUMTAKA SANE



**LONDON,** England

CHELSEA inatarajia kumsajili, Leroy Sane kutoka kwa mabingwa wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, Bayern Munich, kwa mujibu wa Express.

Sane aliondoka Manchester City kwenda Bayern Munich mwaka 2020, hata hivyo, mambo hayajakwenda kama yalivyotarajiwa kwa nyota huyo wa Ujerumani.


Na sasa Chelsea imeripotiwa kujaribu kumrudisha Sane kwenye Ligi Kuu England.

Sane maisha yake kule Bayern yamekuwa magumu na kushindwa kupata nafasi ya kucheza mara kwa mara katika kikosi cha kwanza.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, kocha wa Chelsea ambao ni mabingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, Thomas Tuchel, anamuwania Sane ambaye ni raia mwenzake wa Ujerumani.

Sane alipotua Bayern, alilazimika kukaa karibu msimu mzima bila kucheza, baada ya kuumia goti.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa, dili hilo la Sane litawahusisha wachezaji wengine kama Callum Hudson-Odoi, Hakim Ziyech au Christian Pulisic.



# *Ronaldo alitaka taji la EPL na Man United*

**MANCHESTER,** England

CRISTIANO Ronaldo ameiambia klabu ya Manchester United kuwa wanahitaji kushinda taji la Ligi Kuu England msimu huu, akiwa amerejea klabuni hapo baada ya miaka 12.

Nyota huyu kwa sasa ameshatua jijini Manchester, baada ya kuruhusiwa kuondoka mapema kwenye kibarua cha timu ya Taifa ya Ureno, na sasa anatimiza sharti la lazima la kujitenga kwa siku 14 karantini kutokana na corona.

Nyota huyo amerejea Man United wakiwa tayari wameshakusanya pointi saba kati ya tisa kwenye Ligi Kuu msimu huu wa 2021/22, kwa sasa wapo nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Kwa mujibu wa gazeti la Sun, mshindi huyu mara tano wa Ballon d'or, amewaambia wachezaji wenzake kuwa ana hamu kubwa ya kupata ushindi huo sasa na ni wakati wa klabu hiyo kushinda.

Chanzo kutoka ndani ya klabu kimeripoti, kuwa wachezaji wamefurahi kumpokea Ronaldo hapo Man United na wameona wamepata morali na ujasiri zaidi.

Chanzo kinasema kuwa wachezaji na makocha kwa sasa wanaamini kuwa wana kikosi bora zaidi kwenye ligi na wanaweza kutwaa taji.

LIVE IN PLAY
BET MECHI IKIENDELEA USHINDE.

SPORTPESA APP
CHEZA, USHINDE. MALIPO FASTA




# MANCINI KUFANYA MABADILIKO



**ROME,** Italia

ROBERTO Mancini anapanga kukifanyia mabadiliko kikosi cha kwanza cha Italia kwa mchezo ujao, baada ya kutoka suluhu na Uswisi, Jumapili.

'Azzurri' hao walitengeneza nafasi nyingi na penalti ya Jorginho iliyookolewa na golikipa, Yann Sommer, ambaye aliokoa hatari saba kwenye mchezo huo uliopigwa Uwanja wa St. Jakob-Park.

Ulikuwa ni mchezo wa pili kutoka sare kwa mabingwa hao wa Euro 2020, ndani ya siku tatu baada ya kufungana bao 1-1 na Bulgaria kwenye kufuzu michuano ya Kombe la Dunia Qatar 2022.

Licha ya kutobeba pointi nyingi, Italia walifikisha mechi 36 bila kupoteza, wakifikia rekodi ya Brazil iliyowekwa mwaka 1993 na 1996 ya kucheza mechi bila kupoteza.

Mancini hakuridhishwa na kiwango cha timu yake kwa kutofunga mabao na sasa anapanga kufanya mabadiliko.

"Huu ni wakati ambao mpira unatakiwa kuingia tu kwenye nyavu," alisema Mancini akiiambia Rai Sport.

"Kwa mara nyingine, tulikuwa na nafasi nyingi kwenye mchezo na tukashindwa kushinda."

Sare ya Jumapili iliwaacha Italia kuwa na pointi nne mbele ya Uswisi katika Kundi C, lakini wana mechi mbili mkononi.



# Lukaku akataa kufananishwa

**BRUSSELS,** Ubelgiji

STRAIKA wa Chelsea, Romelu Lukaku, anafurahi kumwona Cristiano Ronaldo amerudi kwenye Ligi Kuu England, lakini kamwe hatathubutu kulinganisha rekodi yake na ile ya mshambuliaji huyo wa Manchester United.

Ronaldo aliandika historia Jumatano iliyopita kwa kuwa mfungaji bora wa muda wote kwenye timu za taifa.

Ronaldo alifunga mabao mawili ya kichwa kwa timu yake wakati wa mechi za kufuzu Kombe la Dunia wakishinda 2-1, dhidi ya Jamhuri ya Ireland na kumpita Ali Daei aliyekuwa anashikilia rekodi ya kufunga mabao 109.

Mabao 111 ya mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or yametokana na mechi 180.

Hiyo inalinganishwa na wastani wa mabao 0.66, kwa kila mchezo kwa Lukaku katika timu ya taifa, mwenye umri wa miaka 28, akiwa amefunga mara 66 katika mechi 99 za Ubelgiji kwenye mashindano yote.

Wakati Lukaku bado ana muda mwingi kwa upande wake kuweza kufukuzia rekodi ya Ronaldo, mshambuliaji huyo hodari hapendelei sifa za binafsi juu ya heshima ya timu.

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMANNE - 07 - SEPTEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 4062 | South Korea vs Lebanon | 1.13 | 6.59 | 16.47 |
| 15:00 | 4042 | Vietnam vs Australia | 12.62 | 5.83 | 1.18 |
| 16:00 | 1964 | Tanzania vs Madagascar | 2.35 | 2.85 | 3.14 |
| 16:00 | 4546 | Zambia vs Tunisia | 3.81 | 2.85 | 2.08 |
| 16:00 | 4970 | Malawi vs Mozambique | 2.90 | 2.85 | 2.75 |
| 16:30 | 3319 | ACS Somuz Falticeni vs CS Aerostar Bacau | 2.52 | 3.49 | 2.43 |
| 16:30 | 3747 | AFC Odorheiu Secuiesc vs Hermanstadt | 3.67 | 3.57 | 1.84 |
| 16:30 | 4088 | Acso Filiasi vs ACS Sirineasa | 2.80 | 3.29 | 2.30 |
| 16:30 | 4895 | CS Soimii Lipova vs Politehnica Timisoara | 3.73 | 3.63 | 1.81 |
| 17:00 | 2551 | Brasil Pelotas RS vs Confianca SE | 2.31 | 2.91 | 3.15 |
| 18:00 | 4051 | Zaglebie II Lubin vs Foto Higiena Gac | 1.74 | 3.88 | 3.83 |
| 18:00 | 5902 | China vs Japan | 10.62 | 5.60 | 1.22 |
| 18:30 | 3284 | Hifk vs Seinajoen JK | 2.90 | 2.85 | 2.51 |
| 18:30 | 5843 | FC Ilves-Kissat vs Kaapo Kaarina | 2.42 | 3.80 | 2.60 |
| 19:00 | 1439 | Azerbaijan vs Portugal | 19.03 | 7.61 | 1.14 |
| 19:00 | 2305 | Ethiopia vs Zimbabwe | 2.26 | 2.95 | 3.19 |
| 19:00 | 2715 | Cape Verde vs Nigeria | 2.95 | 2.85 | 2.47 |
| 19:00 | 2722 | Syrian Arab Republic vs United Arab Emirates | 3.05 | 3.05 | 2.28 |
| 19:00 | 2772 | Stromsgodset 2 vs Fredrikstad FK 2 | 1.94 | 3.89 | 3.11 |
| 19:00 | 3876 | Oman vs Saudi Arabia | 4.75 | 3.39 | 1.70 |
| 19:00 | 3990 | Congo vs Senegal | 5.04 | 3.10 | 1.74 |
| 19:00 | 4966 | Kiffen vs Atlantis FC | 3.00 | 3.63 | 2.06 |
| 19:00 | 5292 | Equatorial Guinea vs Mauritania | 2.21 | 3.09 | 3.14 |
| 20:00 | 2967 | Ayr United vs Raith Rovers | 3.18 | 3.38 | 2.11 |
| 20:30 | 4673 | Fjolnir vs Vestmannaeyjar | 2.76 | 3.63 | 2.19 |
| 21:00 | 1188 | Melipilla vs Union Espanola | 2.36 | 3.48 | 2.61 |
| 21:00 | 2400 | England U21 vs Kosovo U21 | 1.04 | 9.67 | 29.02 |
| 21:00 | 3734 | Doncaster vs Rotherham | 3.29 | 3.34 | 2.03 |
| 21:00 | 5120 | Iraq vs Iran | 4.53 | 3.18 | 1.78 |
| 21:30 | 3101 | Northern Ireland U21 vs Slovakia U21 | 3.30 | 3.55 | 2.10 |
| 21:30 | 4410 | Colchester vs Gillingham | 2.76 | 3.20 | 2.38 |
| 21:30 | 4691 | San Marino U21 vs Hungary U21 | 33.69 | 10.59 | 1.03 |
| 21:45 | 2067 | Bosnia and Herzegovina vs Kazakhstan | 1.22 | 5.82 | 14.05 |
| 21:45 | 2210 | AFC Wimbledon vs Portsmouth | 2.86 | 3.20 | 2.31 |
| 21:45 | 2217 | Slovakia vs Cyprus | 1.43 | 4.49 | 7.38 |
| 21:45 | 2307 | France vs Finland | 1.18 | 6.61 | 16.02 |
| 21:45 | 2366 | Croatia vs Slovenia | 1.61 | 3.85 | 5.60 |
| 21:45 | 2961 | Norway vs Gibraltar | 1.01 | 17.97 | 79.86 |
| 21:45 | 3714 | Russia vs Malta | 1.12 | 8.57 | 20.94 |
| 21:45 | 3854 | Faroe Islands vs Moldova | 2.31 | 2.95 | 3.46 |
| 21:45 | 4625 | Austria vs Scotland | 1.82 | 3.49 | 4.49 |
| 21:45 | 5082 | Ireland vs Serbia | 3.36 | 3.31 | 2.17 |
| 21:45 | 5146 | Montenegro vs Latvia | 1.44 | 4.31 | 7.41 |
| 21:45 | 5523 | Denmark vs Israel | 1.29 | 5.40 | 10.00 |
| 21:45 | 5721 | Netherlands vs Turkey | 1.35 | 5.19 | 7.98 |
| 21:45 | 5772 | Leamington vs Gateshead | 2.72 | 3.44 | 2.29 |
| 22:00 | 1151 | Angola vs Libya | 2.06 | 3.06 | 3.54 |
| 22:00 | 1721 | Burkina Faso vs Algeria | 6.78 | 3.73 | 1.47 |
| 22:00 | 4930 | Sudan vs Guinea Bissau | 1.99 | 3.05 | 3.77 |
| 23:30 | 4614 | Antofagasta vs Curico Unido | 2.05 | 3.34 | 3.24 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# UTATA MECHI YA BRAZIL, ARGENTINA IKIVUNJIKA

## ●●● Fifa yasubiri ushahidi kuamua baada ya polisi kuvamia uwanjani kuwatoa wachezaji...

**SAO PAULO,** Brazil

MCHEZO kati ya Brazil na Argentina kuwania kufuzu michuano ya Kombe la Dunia iliahirishwa ikiwa ni dakika sita tangu uanze juzi, Jumapili.

Hiyo ni baada ya maofisa wa afya wa Brazil kubaini kuwa wachezaji watatu, ambao walianza kwenye kikosi cha Argentina hawakufuata kanuni za kukaa karantini kutokana na corona.

Wachezaji watatu wa Argentina walivunja sheria ya nchini Brazil ya kuwataka kukaa karantini kwa siku 14, kwa wageni wote wanaoingia nchini humo wakitokea England.

**Wageni Argentina walitoka kwenye Uwanja wa Corinthians Arena baada ya maofisa wa Brazil kusimamisha mchezo huo.**

Ingawa wachezaji hao hawakutajwa, lakini kuna nyota wanne wa Argentina wanaochezea klabu za Ligi Kuu England ambazo ni Emiliano Buendia na Emiliano Martinez wanaoichezea Aston Villa, na Giovani lo Celso na Cristian Romero wa Tottenham Hotspur.

Martinez, Lo Celso na Romero wote walianza kwenye mchezo huo uliopigwa hapa jijini Sao Paulo.

Bado haijatajwa tarehe rasmi ya kurudiwa kwa mchezo huo na Argentina waliondoka na kurudi nyumbani, kwa ajili ya kujiandaa na mchezo mwingine wa kufuzu Kombe la Dunia dhidi ya Bolivia utakaopigwa Ijumaa ya Septemba 10, mwaka huu.

Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), linasubiri ushahidi wa sababu za kusitishwa kwa mchezo huo, kabla ya kuchukua hatua.

## ZISIKUPITE

### SALAH ABEMBELEZWA LIVER

LIVERPOOL wanaendelea kuzungumza na wawakilishi wa Mohamed Salah kuhusu mkataba mpya wa mshambuliaji nyota huyo wa Misri mwenye umri wa miaka 29. ***(Liverpool Echo)***

### JAMES ATAKIWA UTURUKI

KIUNGO wa kati wa Everton na Colombia, James Rodriguez amehusishwa na uhamisho wa kwenda Istanbul Basaksehir, klabu hiyo ya Uturuki inapania kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30- kabla ya dirisha lao la uhamisho kufungwa Jumatano wiki hii. ***(Footmercato)***

### SEVILLE HAIKUMZUIA KOUNNDE

KOCHA wa Sevilla, Julen Lopetegui, amesema klabu hiyo ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga haikuwa na nia mbaya ya kumzuia beki Mfaransa, Jules Kounde mwenye umri wa miaka 22, kuhamia Chelsea msimu huu wa joto, lakini ni muhimu kwake kubaki. ***(Mirror)***

### ONANA KUTUA ARSENAL

MKURUGENZI wa soka wa Ajax, Marc Overmars, amesema kipa wa Cameroon, Andre Onana mwenye umri wa miaka 25, ambaye anasakwa na Arsenal, huenda akaondoka msimu ujao kwa uhamisho huru. ***(Team Talk)***

### ONANA AHUSISHWA NA INTER

BINGWA mtetezi wa Italia, Inter Milan pia wanahusishwa na Andre Onana, ambaye anatajwa kwenda kurithi mikoba ya kipa wa Slovenia, Samir Handanovic mwenye umri wa miaka 37. ***(Calciomercato)***

### PSG WAKOMAA NA MBAPPE

KLABU ya Paris St-Germain ina matumaini kwamba, mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe atajitolea kikamilifu kutekeleza mkataba wake mpya licha ya azma ya nyota huyo mwenye umri wa miaka 22, kutaka kujiunga na Real Madrid kwa uhamisho wa bure msimu ujao. ***(Athletic)***

### ARSENAL KUMPOTEZA NKETIAH

ARSENAL inakabiliwa na hatari ya kupata hasara kubwa baada ya kushindwa kumuuza mshambuliaji wa miaka 22, Eddie Nketiah, huku mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa England wa chini ya miaka 21, akikataa ofa ya kandarasi kutoka kwa 'Washikabunduki' hao. ***(Sun)***

### O'BRIEN NA MKATABA MPYA

KIUNGO wa kati wa Huddersfield Town, Lewis O'Brien mwenye umri wa miaka 22, ambaye pia alitakiwa na Leeds United msimu uliopita, anajadiliana kuhusu mkataba mpya. ***(Huddersfield Examiner)***

### LAPORTA AMUAGIZA KOEMAN

KOCHA wa Barcelona, Ronald Koeman, ameambiwa na Rais wa klabu hiyo, Joan Laporta, kuwatumia zaidi kiungo wa Hispania, Riqui Puig mwenye umri wa miaka 22 na Samuel Umtiti mwenye miaka 27. ***(Marca)***

## Simba Queens yakwama CAF

**Na Somoe Ng'itu,** NAIROBI

TIMU ya Simba Queens, imeshindwa kutinga fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Ukanda wa CECAFA baada ya kukubali kuchapwa mabao 2-1 na wenyeji, Vihiga Queens ya Kenya katika mechi ya hatua ya nusu fainali iliyochezwa kwenye Uwanja wa Nyayo jijini hapa jana mchana.

Kwa matokeo hayo, Simba Queens sasa itacheza mechi ya kusaka mshindi wa tatu na timu itakayopoteza mchezo wa nusu fainali ya pili iliyowakutanisha Lady Doves ya Uganda na Commercial Bank of Ethiopia.

Maureen Achieng aliifungia Vihiga Queens bao la kwanza dakika 65 kwa kichwa akiunganisha mpira wa kona baada ya mabeki wa Simba Queens kujichanganya kuzuia shambulizi hilo, lakini Aisha Juma aliyeingia kuchukua nafasi ya Violeth Nicholas baada ya kuumia, aliwasawazishia mabingwa hao wa Tanzania dakika ya 83.

Bao la pili la Vihiga Queens lilifungwa pia kwa kichwa na Jentrix Shikangwa baada ya kuruka na kuunganisha krosi huku kipa wa Simba Queens, Zubeda Mgunda akishindwa kudaka na mpira kutinga wavuni dakika ya 88.

## JWTZ watakiwa kumulika Olimpiki

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

JESHI la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), limetakiwa kuongeza wigo wa michezo wakati wa mashindano ya shule za sekondari zilizo chini ya jeshi hilo, ili kulisaidia taifa kusonga mbele kimichezo, hasa kwa kuangalia fursa za michezo zaidi ya 400 iliyoshindaniwa kwenye michuano ya Olimpiki mwaka huu.

Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Anga mstaafu, Meja Jenerali George Ingram, ndiye aliyetoa rai hiyo wakati akifungua awamu ya sita ya michuano ya michezo kwa shule zinazomilikiwa na JWTZ, inayoendelea katika Shule ya Sekondari Kizuka, iliyopo wilayani Morogoro, ambapo alisema michezo minne inayochezwa mwaka huu ni michache ikilinganishwa na fursa ya michezo mingi iliyopo kimataifa.

Ingram alisema shule za sekondari zinazomilikiwa na jeshi ni hodari katika kutoa wanamichezo wazuri kwenye Umoja wa Michezo kwa Shule za Sekondari (UMISETA), na kuwika katika timu mbalimbali nchini, huku wengine wakipata ajira za kudumu katika taasisi, kampuni na mashirika mbalimbali.

# MSHINDI 'KAPU LA WANA' PILSNER LAGER AFUNGUKA

**Na Mwandishi Wetu**

MSHINDI wa kwanza wa Promosheni ya 'Kapu la Wana' inayoendeshwa na Bia ya Pilsner Lager, mkulima wa Kijiji cha Kabutoto wilayani Muleba, Kagera, Privatus Mujuni, amesema zawadi ya Power Tiller aliyoshinda ni nyenzo muhimu kwa shughuli zake za kilimo na kwamba itakwenda kubadilisha maisha yake.

**Akizungumza muda mfupi baada ya kukabidhiwa zawadi hiyo wilayani Muleba, Mujuni alisema amekuwa akishindwa kulima shamba kubwa kutokana na kukosa mtaji hususan fedha za kulipa trekta la kulimia na kwamba Power Tiller aliyopata ni ufunguo wa mafanikio kwake.**

"Hakika maisha yangu hayawezi kuwa kama yalivyokuwa kabla ya kupata zawadi hii, ambayo ni nyenzo muhimu sana kwa kazi yangu. Kutokana na kukosa mtaji nilikuwa nalima kwa jembe la mkono na nikijitahidi sana naishia kulima heka tatu na nusu. Baada ya kupata hii Power Tiller, malengo yangu sasa ni kulima heka 10," alisema.

Sambamba na kulima shamba kubwa zaidi, Mujuni alisema kuna uhitaji mkubwa wa matreka ya kulimia kijijini kwake na kwamba atatumia Power Tiller hilo kulima mashamba ya wanakijiji watakaohitaji huduma hiyo na kujipatia kipato, kwa ajili ya kuendesha maisha yake na familia huku akiishuru bia ya Pilsner Lager kwa kumpa zawadi itakayobadilisha maisha yake.

Mkuu wa Wilaya ya Mubela, Toba Nguvila, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika hafla ya kukabidhi zawadi hiyo kwa mshindi, alisema vijana wanapaswa kuchangamkia fursa kupitia promosheni hiyo kama alivyofanya Mujuni, ili kupata zawadi zitakazowafanya wapige hatua kwenye shughuli wanazofanya.

"Kwanza niishukuru sana bia ya Pilsner Lager kwa kuja na promosheni hii inayobadilisha maisha ya vijana wapambanaji kama Mujuni. Kikubwa ni vijana kuchukua hatua kwa kushiriki ili waweze kushinda na kupata zawadi zitakazoweka alama katika maisha yao," alisema.

Meneja Mauzo wa Kampuni ya Serengeti Breweries (SBL), watengenezaji wa bia hiyo, kwa upande wa Mwanza, Patrick Kisaka, alisema kampuni hiyo itawawezesha washindi watano kutoka Kanda ya Kati, Kusini, Kaskazini, Pwani na Kanda ya Ziwa kuwa sehemu ya zawadi zenye thamani ya mpaka milioni 50 itakayotolewa, kwa kila mshindi kuweza kujishindia vitendea kazi vyenye thamani ya milioni kumi zitakazowawezesha kuboresha biashara wanazofanya na kutimiza ndoto zao.

Kwa mujibu Kisaka, shindano hilo ni mahususi kwa ajili ya vijana wapambanaji wanaofanya shughuli mbalimbali kama ukulima, uvuvi, vinyozi, waendesha bodaboda na wengineo, ambao wanatamani kufikia malengo makubwa, lakini wanapata changamoto katika upambanaji wao kutokana na kukosa uwezeshwaji hali inayowapunguzia kasi ya kufikia malengo yao na mafanikio kwa wakati.



Msanii wa ngoma za asili, Saida Karol (wa pili kulia aliyetinga mavazi meusi) akitumbuiza pamoja na kundi lake wakati wa kukabidhi zawadi ya Power Tiller kwa mshindi wa kwanza wa Promosheni ya 'Kapu la Wana' inayoendeshwa na Bia ya Pilsner Lager, iliyofanyika Muleba mkoani Kagera. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Azam walia ratiba Fifa kuwatibulia Zambia*

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa timu ya Azam umesema ratiba ya Shirikisho la Soka duniani (Fifa), imeharibu mipango yao ya maandalizi ya msimu ujao baada ya kuwakosa nyota 10, ambao walikuwa kwenye majukumu ya timu zao za taifa.

Azam FC imerejea nchini jana ikitokea Ndola, Zambia, ilipoweka kambi kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, CAF.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa Azam FC, Zakaria Thabiti 'Zaka Zakazi', alisema kikosi chao kimerejea nchini baada ya kutoka Zambia, walipokuwa wakijiandaa na msimu mpya, lakini mambo hayakwenda kama ilivyotarajiwa kutokana na uchache wa wachezaji.

Alisema walikuwa na wachezaji 19 pekee badala ya 29, jambo ambalo lilikwamisha maandalizi yao kwenda kama walivyotarajia.

"Kambi ilikuwa na mafanikio makubwa kwa kupata kile kinachohitajika kwa kucheza mechi za kirafiki, zimempa mwaga kocha Lwandamina (George) kuona mapungufu yake, lakini hakuweza kupata mazoezi ya kimbinu kwa sababu ya kuwapo kwa uchache wa wachezaji," alisema Zaka.

Alisema wamerejea nchini kuendelea na mazoezi ya kawaida kujiandaa na mchezo wao dhidi ya Horseed SC ya Somalia, kuhakikisha wanapata matokeo mazuri.

Azam FC watacheza mechi ya kwanza Jumamosi wiki, katika Uwanja wa Azam Complex na mchezo wa marudiano utapigwa kwenye dimba la Uhuru jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki ijayo.

Michezo
Jumanne Septemba 7, 2021
Nipashe



Lukaku akatae kufananishwa
UKURASA 21

NIPO FITI...



Mshambuliaji wa Taifa Stars, Mbwana Samatta akiwa mazoezini Uwanja wa Benjamin Mkapa na Kocha Mkuu wa timu hiyo, Kim Poulsen jana, kuelekea mechi ya leo dhidi ya Madagascar kuwania kufuzu Kombe la Dunia 2022. **PICHA: TFF**

## Yanga yashtukia Wanaigeria

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imesema imewashtukia baadhi ya watu ambao ni mashushushu wa klabu ya Rivers United ambao wamekuja kwa kazi ya kuipeleleza na kuangalia mechi zao watakazocheza.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli, amesema watu hao wapo Dar es Salaam na wamekuwa wakiwafuatilia, lakini nao wamekuwa makini kwani wamewagundua.

Bumbuli alisema kutokana na umakini walionao ndiyo maana wamekuwa hawachezi mechi za wazi ambazo mashabiki au kila mtu atakwenda kuziangalia, ili kuepuka mashushushu hao kusoma mbinu za kocha wao Nasreddine Nabi.

"Tumegundua kuwa wenzetu wameleta mashushushu wao. Lengo lao ni kutupeleleza, tupo vipi, waangalie mechi zetu ili kujua udhaifu wetu uko wapi. Lakini hili tumeligundua," alisema.

Yanga ambayo ilicheza mechi kwenye kilele cha Wiki ya Wananchi Agosti 29, imecheza mechi zake mbili bila mashabiki dhidi ya Friends Ranger na kushinda mabao 3-1, lakini juzi ilicheza dhidi ya Pan African na kuichapa bao 1-0.

"Mwalimu anasema bado anaendelea kukisuka kikosi, lakini amesema mpaka Jumatano ama Alhamisi atakuwa kwenye mwanga mzuri, kwa sababu atakuwa na kikosi chake chote pamoja na wachezaji walikwenda kwenye vikosi vya timu ya taifa. Baada ya mechi dhidi ya Pan African, mwalimu amewapa mapumziko wachezaji wetu na kesho jioni. Ameamua kufanya hivyo kwa sababu baada ya hapo sidhani kama watakuwa tena na nafasi hiyo, kwani baada ya mechi dhidi ya Rivers United kuna safari ya kwenda nchini Nigeria, hivyo hawatokuwa na mapumziko," alisema Bumbuli kuelekea mechi hiyo ya Jumapili katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

# QATAR YAIOMBEA STARS IFUZU KOMBE LA DUNIA

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

## Madagascar yasema inataka pointi tatu leo, Poulsen naye afunguka na kumtaja Samatta...

WAKATI Taifa Stars ikishuka Uwanja wa Benjamin Mkapa leo kuikaribisha Madagascar kwenye mechi ya kuwania kufuzu fainali za Kombe la Dunia 2022, waandaji wa michuano hiyo, Qatar wameiombea Tanzania kupata ushindi na hatimaye kufuzu fainali hizo.

**Akizungumza kwenye Ofisi za Kampuni ya Magazeti ya The Guardian Ltd jana, Ofisa wa Ngazi za Juu wa Ubalozi wa Qatar nchini, Hamad Al Dosari, alisema anaitakia kila la kheri Stars ishinde mechi ya leo dhidi ya Madagascar, lakini ifanikiwe kufuzu kwenye fainali hizo za mwakani.**

"Nawatakia ushindi leo, lakini nina imani kuwa Tanzania inaweza kufuzu kwenye fainali hizo, nawatakia kila la kheri," alisema.

Mbali na hayo, alisema kuwa Tanzania itanufaika na vitu vingi kutokana na wenyeji wa Qatar kwenye fainali hizo, ikiwamo vifaa mbalimbali vitakavyotumika kwenye michuano hiyo baada ya kumalizika.

"Baada ya Kombe la Dunia kumalizika, vifaa vitakavyotumika tutavigawa kwenye nchi jirani ambazo zipo karibu kijiografia za Kiafrika, ikiwamo Tanzania," alisema ofisa huyo. Katika ziara yake ya kutembelea vyombo vya habari vya IPP, Dosari alisema ubalozi huo uko tayari kushirikiana na vyombo vya habari nchini kufanikisha baadhi ya waandishi kwenda nchini humo kuripoti fainali hizo.

Katika hatua nyingine, kuelekea mchezo huo wa leo, Kocha Mkuu wa Stars, Kim Poulsen, amesema anatarajia utakuwa mgumu kutokana na ubora wa Madagascar, ambao timu yao imekaa pamoja kwa muda mrefu, hivyo ushindani utakuwa mkubwa.

"Katika mazoezi ya mwisho tuliyofanya wachezaji wote wako vizuri hatuna majeruhi yeyote ila tunapaswa kucheza kwa nguvu ili tuweze kupata matokeo.

"Lakini kuna uwezekano mkubwa wa kufanya mabadiliko ya wachezaji kutokana na aina ya wapinzani wetu, nimefurahi kumwona Samatta [Mbwana] ni mchezaji mzuri anayecheza soka la kulipwa Ulaya nitaangalia kama ninaweza kumtumia " alisema Poulsen.

Kocha Mkuu wa Madagascar, Eric Rabesandratana, alisema wamejipanga kurekebisha makosa katika mchezo dhidi ya Tanzania baada ya kukubali kufungwa nyumbani na Benin.

"Tumeangalia video nyingi za Tanzania ni timu nzuri, tunaamini tutaenda kupata upinzani wa nguvu kutokana na ubora wa timu yao, tutaenda kuwakosa baadhi ya wachezaji wa kikosi cha kwanza, lakini tumepanga kuhakikisha tunaondoka na pointi tatu," alisema Eric.

Tanzania ambayo ilitoka sare ya bao 1-1 kwenye mechi ya kwanza ugenini dhidi ya DR Congo, ipo nafasi ya 135 kwenye viwango vya Fifa wakati Madagascar iliyopigwa 1-0 nyumbani dhidi ya Benin, ipo nafasi ya 97 kwenye viwango hivyo duniani.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002